# Kitini cha mgogoro wa mabadiliko ya tabia nchi kwa vyombo vya habari Tanzania



# Kitini cha mgogoro wa mabadiliko ya tabia nchi kwa vyombo vya habari Tanzania


**Utangulizi** p.01-03

**Kifungu cha 1**: Sehemu ya 1 Uandishi wa mabadiliko ya tabia nchi: Wapi pa kuanzia? p.04-14

**Kifungu cha 2**: Usimuliaji wa Hadithi: Kuifanya hadhira kujali kuhusu mabadiliko ya tabia nchi p.15-25

**Kifungu cha 3**: Upotoshaji kuhusu mabadiliko ya tabia nchi: Kuielimisha hadhira p.26-34

**Kifungu cha 4**: Kuripotia mabadiliko ya tabia nchi kwa usalama p.35-48

**Kiambatanisho cha 1**: Hadhira yangu ni nani? Maswali ya Dodoso p.49

**Kiambatanisho cha 2**: Fomu ya Tathmini ya viashiria vya Hatari p.50

**Kiambatisho cha 3**: Marejeo ya Nyaraka za Kisheria p.51

# Utangulizi

Mwezi Septemba 15, 2025, mwanariadha wa mbio za masafa marefu Alphonce Felix Simbu aliingia katika vitabu vya historia wakati akivuka mstari wa mwisho jijini Tokyo. Alikuwa mwanariadha wa kwanza wa Tanzania kushinda medali ya dhahabu ya Mashindano ya Mbio Ulimwenguni katika matukio yote ya mbio za masafa mafupi na marefu. Kinachomfanya kupata mafanikio yake kuwa ya kuvutia zaidi ni ushuhuda alioutoa wakati wa mahojiano mwaka mmoja kabla ya mashindano hayo ambapo alinukuliwa akisema: "hali ya hewa ilikuwa baridi mno miaka kumi iliyopita, lakini sasa ni vigumu mno kufanya mazoezi wakati wa mchana kutokana na joto kali. Kwa sasa nafanya mazoezi wakati wa jioni, na hii inamaanisha kuwa muda wa mazoezi umekuwa mfupi." 1

Mabadiliko ya tabia nchi siyo jambo la wanasayansi tu na wanasiasa: yanaathiri wanariadha wa mbio za kulipwa pia. Kama ukiangalia kwa karibu zaidi utagundua kuwa mgogoro wa mabadiliko ya tabia nchi unaathiri kila kitu katika chumba cha habari, kuanzia kwenye michezo hadi kwenye afya, kuanzia kwenye elimu hadi kwenye serikali za mitaa na zaidi ya hapo.

### Lengo la kitini hiki ni kukusaidia wewe kama mwandishi wa habari na mhariri:

- **Kuwajengea uwezo watumiaji wako wa maudhui.** Tafuta uhusiano uliopo na mabadiliko ya tabia nchi kwenye habari zako za kila siku ili kuwashirikisha na kuwapa uwezo watumiaji wako wa maudhui kupata taarifa wanazohitaji, kuwasaidia kulinda vyanzo vyao vya kipato na mustakabali wa maisha ya baadaye kutokana na hali mbaya ya hewa
- **Kukuza uwajibikaji**. Kuwawajibisha wenye mamlaka kutokana na maamuzi wanayoyafanya ambayo yanahusiana na au yanaongeza athari za mabadiliko ya tabia nchi
- **Kuongeza ujuzi:** Kuongeza uwezekano wako wa kuajiriwa kutokana na kuwa na uwezo wa kutafsiri masuala ya mabadiliko ya tabia nchi, kujenga, kushirikisha na kuwashikilia watumiaji wa maudhui kwenye chombo cha habari

Kitini kimegawanyika katika maeneo makuu manne yaliyo na ushauri wa wataalamu, mafunzo kwa mifano na kwa vitendo. **Mwisho wa Kitini hiki utaweza:**

- Kuandaa habari za mabadiliko ya tabia nchi zenye kuvutia watumiaji kwa kutumia mbinu mbalimbali za kusimulia habari
- Kutambua jinsi waandishi wa habari wanavyoweza kukabiliana na kusambaa kwa taarifa za uongo na za uzushi juu ya mabadiliko ya tabia nchi na umuhimu wa kukabiliana na taarifa hizo
- Kutambua jinsi ya kurahisisha lugha ya kisayansi kuhusu mabadiliko ya tabia nchi na hivyo taarifa kuweza kuwafikia watumiaji wa maudhui ya vyombo vya habari nchini Tanzania kwa urahisi
- Kutambua umuhimu wa kufanya tathmini ya hatari inayoweza kujitokeza ili kubakia salama kimwili na mtandaoni
- Kutambua zaidi kuhusu jinsi mifumo ya sheria inavyowaathiri waandishi wa habari nchini Tanzania

*Kumbukumbu:* [1] https://dialogue.earth/en/climate/how-climate-change-is-impacting-sports-in-africa/

## Kuangazia mabadiliko ya tabia nchi nchini Tanzania

Wewe ni mwandishi wa habari na hivyo kuwa msimuliaji wa habari lakini kabla hujaanza kusimulia habari unapaswa kuelewa na kuwa na ufahamu wa nini unakisimulia.

Hii ina maana kuwa unahitaji kutambua na kuwa na uwezo wa kuelezea madhara ya mabadiliko ya tabia nchi katika maisha na vyanzo vya kipato kwa watu wa Tanzania sasa na pengine katika nyakati zijazo.

Benki ya Dunia imeitaja Tanzania kama taifa la Afrika Mashariki linaloathirika zaidi na mafuriko na kuonya kuwa "*Mabadiliko ya tabia nchi yanaathiri zaidi watu wenye uwezo mdogo wa kukabiliana nayo, na kwamba bila kuchukua hatua, watu milioni 2.6 wanaweza kusukumizwa katika kundi la watu maskini ifikapo mwaka 2050*."[2]

Unaweza kufikiri kuwa jinsi matukio mabaya ya hali ya hewa yanavyojitokeza mara kwa mara ndivyo maarifa juu ya mabadiliko ya tabia nchi yanavyozidi kusambazwa. Lakini utafiti wa mwaka 2025 uliofanywa na asasi ya Afrobarometer unadai kuwa ni asilimia 38 tu ya Watanzania wamewahi kusikia neno 'mabadiliko ya tabia nchi'3. Maarifa ni muhimu kwani yanawapa watu uwezo wa kuwa na udhibiti zaidi wa Maisha yao: kwa kutambua hatari inayowakabili na nini wanaweza kufanya vizuri zaidi kulinda makazi na vyanzo vyao vya kipato.

Kitini cha Mabadiliko ya Tabia Nchi kinakupatia fursa kujazia pengo hilo la maarifa na kujenga jamii yenye ufahamu nchini Tanzania.

Kitini hiki kimeandaliwa na asasi ya Thomson Foundation kwa kushirikiana na Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania (Tanzania Media Foundation- TMF), Mtandao wa Kuchukua Hatua dhidi ya Mabadiliko ya Tabia Nchi Tanzania (Climate Action Network Tanzania - CAN TZ), Mtandao wa radio za kijamii Tanzania (Tanzanian Development Information Organization -TADIO), Mtandao wa Wanahabari wa Vyombo vya Mtandaoni (JUMIKITA) na Shirika la Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (Journalists' Environmental Association of Tanzania - JET). Kitini hiki ni sehemu ya mpango wa Wajibika nchini Tanzania unaoongozwa na asasi ya Oxford Policy Management (OPM) na kufadhiliwa na Ofisi ya Masuala ya Kigeni, Jumuiya ya Madola na Maendeleo ya Uingereza (UK's Foreign, Commonwealth and Development Office - FCDO) na Ubalozi wa Uswisi Nchini Tanzania. Mpango huu umeandaliwa kuimarisha uandishi wa masuala ya hali ya hewa, kujengea uwezo vyombo vya habari na kuhakikisha ubora na uendelevu katika kuandika masuala ya mabadiliko ya tabia nchi.

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

**Embassy of Switzerland in Tanzania**

UK International Development
Partnership | Progress | Prosperity

[2] www.worldbank.org/en/country/tanzania/publication/ccdr
[3] https://disinfo.africa/ignorance-and-faith-blur-tanzanias-climate-facts-3944ec758ecb

## Wachangiaji



**Sylivester Domasa** ni meneja wa huduma za vyombo vya kidijitali katika Magazeti ya Serikali- Tanzania Standard Newspapers (TSN). Pia ni mwandishi wa habari mahiri wa habari za sayansi na mazingira mwenye uzoefu wa zaidi ya miaka 15.



**Evalilian Massawe** ni mtangazaji wa redio katika Shirika la Utangazaji Tanzania (Tanzania Broadcasting Corporation -TBC). Ni mwanachama wa Mtandao wa Oxford wa Waandishi wa Habari za Mabadiliko ya Tabia Nchi, mpango wa Taasisi ya Reuters ya Mafunzo ya Uandishi wa Habari katika Chuo Kikuu cha Oxford nchini Uingereza.



**Hassan Mhelela** ni mkuu wa kitengo cha Maudhui ya Mtandaoni katika kampuni ya Utangazaji ya Azam (Azam Media Limited) iliyopo jijini Dar es Salaam. Yeye pia ni mkufunzi wa masuala ya habari na mshauri wa jinsi ya kuimarisha usalama wa kimwili na kidijitali.



**Catherine Mackie** ni mhariri wa mafunzo na mawasiliano kutoka asasi ya Thomson Foundation na mhariri wa Kitini. Aliwahi kuwa mwandishi mwandamizi wa shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) na mhitimu wa Mafunzo ya Uandishi wa Habari ya Knight-Wallace katika Chuo Kikuu cha Michigan (Knight-Wallace Journalism Fellowship at the University of Michigan)



**Ernest Sungura** ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) na pia ni Katibu Mkuu wa Chama Cha Mabaraza ya Habari Duniani. MCT chini ya Uongozi wa Bwana Sungura walitoa ushauri wa kisheria kwa ajili ya kitini hiki.

# Sehemu ya 1 - Uandishi wa mabadiliko ya tabia nchi: Wapi pa kuanzia?

### 1.1 – Kuelewa mabadiliko ya tabia nchi

Mabadiliko ya tabia nchi kama mada kwa ajili ya waandishi wa habari inaweza kuleta mashaka. Inaweza kuwa vigumu kujua unaanzia wapi unapokabiliwa na mashaka makubwa yenye mizizi yake kutoka katika sayansi, misamiati na habari za uzushi. Hata hivo, suala hili linaathiri maisha ya watu wengi: kuanzia kwenye uhaba wa maji hadi mafuriko na kukosekana kwa usalama wa chakula na ukame. Hapa ndio sehemu unayopaswa kuanzia. Utajifunza nini maana ya mabadiliko ya tabia nchi, kwa nini ni mada muhimu kwa waandishi wa habari na jinsi gani unaweza kusambaza maarifa hayo kwa watumiaji wako wa maudhui.

### 1.2 - Nini maana ya 'mgogoro wa mabadiliko ya tabia nchi'?

Tabia nchi imekuwa ikibadilika kiuasilia kwa zaidi ya mamilioni ya miaka. Lakini utofauti wa sasa kulingana na wanasayansi wengi wa masuala ya tabia nchi, ni kasi ambayo mabadiliko hayo yanajitokeza na kiwango cha madhara kwa mwanadamu. Wanaonya kuwa, iwapo dunia itaendelea kuongezeka joto inaweza kusababisha mawimbi ya joto, ukame na mafuriko mabaya zaidi.[1]

Hali hii imesababisha kuibuka kwa jina '**mgogoro wa mabadiliko ya tabia nchi**' ambalo limekuwepo tangu miaka ya 1980. Hata Hivyo, dhana inayotumika zaidi ni pamoja na ile iliyotolewa kwenye hotuba ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa wakati wa Mkutano wa Kilele wa Mabadiliko ya Tabia nchi ulimwenguni mwaka 2019.[2]

Mabadiliko ya tabia nchi yanaathiri nchi mbalimbali kwa uzito tofauti tofauti hivyo ni vema kujifahamisha na misimamo inayochukuliwa na makampuni makubwa ya biashara na serikali ya Tanzania na programu zozote maalum wanazoshiriki. Unaweza kupata viunganishi vya machapisho ya mtandaoni kuhusu mabadiliko ya tabia nchi mwishoni kwa Kitini hiki ili kukujengea maarifa. Maarifa hayo yanaweza pia kukusaidia kuwawajibisha wenye mamlaka ili waweze kutekeleza ahadi zao za zamani, za sasa na za siku zijazo.

## Hatua tano za kuelewa mabadiliko ya tabia nchi

**Hatua ya kwanza** - Sayari dunia ina idadi kubwa ya watu kuliko ilivyowahi kuwa katika kipindi chochote kile: zaidi ya watu biloni 8.
**Hatua ya pili** - Maisha yetu yanategemea vyanzo vya nishati mafuta (fuel): mafuta, makaa ya mawe na gesi.
**Hatua ya tatu** - Kuchoma nishati mafuta kunatoa gesi ambayo inanyonya joto kutoka kwenye jua. Na gesi hizi zinajulikana kama hewa ya ukaa.
**Hatua ya nne** - Hewa ukaa ($CO_2$) ni moja ya hewa mbaya zaidi inayosababisha mabadiliko ya tabia nchi. Ukataji wa miti unasababisha hali kuwa mbaya zaidi kwasababu miti inanyonya hewa hii ya ukaa.

[1] https://www.un.org/en/climatechange/science/key-findings
[2] https://www.un.org/sg/en/content/sg/statements/2019-09-23/secretary-generals-remarks-closing-of-climate-action-summit-delivered

**Hatua ya tano** - Madhara ya mabadiliko ya tabia nchi ni pamoja na ukame mkali, uhaba wa maji, moto mbaya wa msituni, kuongezeka kwa kina cha bahari, mafuriko3.

## 1.3 – Hali ya hewa au mabadiliko ya tabia nchi?

Zingatia swali hili. Wewe ni mwandishi wa zamu katika chombo chako cha habari na mvua kubwa inanyesha na kusababisha mafuriko. Je habari yako itakuwa kuhusu hali ya hewa au inaweza kuhusishwa na mabadiliko ya tabia nchi? Nini kitaifanya habari kuwa na uwezekano wa kuhusiana na mabadiliko ya tabia nchi?

Hapa njia rahisi ni: **FIKIRIA KUHUSU WAKATI**

***Hali ya hewa*** inahusiana na hali ya anga ya **muda mfupi** kwa wakati mfupi, masaa kadhaa au siku kadhaa.

***Tabia nchi*** inahusiana na hali ya anga ya **muda mrefu** (mfano., wastani wa joto, mvua, utokeaji wa mara kwa mara na ukubwa wa vimbunga), kwa miaka mingi au miongo.

Hebu turejee katika mazingira ya kwanza. Wewe ni mwandishi wa zamu na mvua kubwa inanyesha na kusababisha mafuriko. Katika habari yako utaiweka kwenye mwelekeo upi:


A. Hali ya hewa
B. Mabadiliko ya tabia nchi
C. Au pengine vyote viwili

Utapata jibu mwisho wa mafunzo haya.

## 1.4 – Je habari yangu inahusu mazingira au mabadiliko ya tabia nchi?

Katika kutazama kwa haraka maneno mazingira na mabadiliko ya tabia nchi yanaweza kuonekana kushabihiana na katika taarifa nyingi za habari yanatumika kwa pamoja. Lakini kuna tofauti isiyo dhahiri.

[3] https://www.un.org/en/climatechange/science/key-findings




Mabadiliko ya tabia nchi ni moja ya taarifa za habari za mazingira na siyo kila habari ya mazingira inahusu mabadiliko ya tabia nchi.

Kwa mfano, uandishi wa mazingira unaweza pia kuhusu habari za viumbe hai na mazingria au masuala yanayohusu uchafuzi wa mazingira na uchafu unaotokana na sumu unaosababishwa na kukua kwa shughuli za kiuchumi. Mchoro hapo chini unaonyesha maeneo yanayohusiana na uandishi wa habari wa mazingira.

Mchoro huu ni muhimu kwako mwandishi wa habari kwani taarifa zako zinafaa kuwa sahihi kama unataka kuaminiwa na watumiaji wa maudhui yako.

### 1.5 - Je naongea na nani?

Kila mwandishi anahitaji kuwa na mtumiaji wa maudhui ya habari yake. Ili kuhakikisha habari yako ya mabadiliko ya tabia nchi inashindana katika soko lenye msongamano wa taarifa za habari unapaswa kumtambua mtumaiji wako wa maudhui ili kutengeneza maudhui ambayo yatawavutia na kuwahabarisha watumiaji kuhusu ni nani na ni nini kinaathiri maisha yao, na hivyo kuwawezesha kutoa maamuzi. Hii inamaanisha kutambua unazungumza na nani. Unaweza kuwa unafanya kazi na redio ya kijamii au chombo cha habari za vijijini. Mahali pa kuanzia popote ulipo ni kutafuta kama chombo cha habari unachofanyia kazi kinakusanya taarifa za kina juu ya watumiaji wake wa maudhui kama vile:

- umri
- jinsia
- mahali wanapoishi
- hali yao ya kijamii na kiuchumi (kipato na kiwango cha elimu)
- tabia zao katika kutumia maudhui (mfano, wakati gani wanaingia mtandaoni, wanatazama habari, wanafungua redio au wapi wanapata taarifa zao)

Watumiaji wako wa maudhui wanaweza kubadilika kulingana na habari au chapisho lako. Kutambua unazunguza na nani, anapendelea nini na wakati gani anatumia majukwaa yako ya habari ni sehemu muhimu ya mkakati wako wa usimuliaji wa habari za mabadiliko ya tabia nchi ambao tutaangazia zaidi katika Sehemu ya 2. Hii itasaidia kubuni, kuunda na kuelekeza ni jinsi gani habari yako itaendana na watumiaji. Kama usipofanya hivyo unaweza kujikuta unaandika au unatangaza kwa ajili yako mwenyewe.



**Sylivester Domasa** ni meneja wa huduma za vyombo vya kidijitali katika Magazeti ya Tanzania Standard Newspapers (TSN). Pia ni mwandishi wa habari mahiri wa habari za sayansi na mazingira. Anasema:

*"Inabidi kuwafikiria watumiaji wangu wa maudhui kila wakati na ninarekebisha na kurekebisha habari yangu karibu muda wote. Kwa nini? Kwasababu tupo nyakati ambapo watu wanatafuta taarifa. Hawatafuti habari … hivyo ni muhimu kujua ni jinsi gani unaandika habari yako ili kuhakikisha mtu anayetafuta katika Mtandao anapata taarifa hiyo?"*

**Mfano:** Utafiti wa kina wa watumiaji wa maudhui ulifanyika kabla na baada ya kuzindua kipindi cha Niambie, kipindi cha redio kinachorushwa kupitia mitandao ya kijamii ambacho kinashirikisha watumiaji wa maudhui kwa kiasi kikubwa, kabla ya kuzinduliwa kwake mwaka 2013. Kiliandaliwa kwa ajili ya vijana na baada ya miaka 10 kimekua hadi kufikia zaidi ya wasikilizaji milioni tano. Tafuta zaidi hapa: https://www.bbc.com/mediaaction/where-we-work/africa/tanzania/celebrating-niambie



*Haki miliki: BBC Media Action*

**Zoezi**: Sehemu yako ya kuanzia ni kujua ni maswali gani unapaswa kuwauliza watumiaji wa maudhui yako. Orodha ya maswali kukusaidia kujifunza zaidi tabia za watumiaji wako inapatikana katika kiambatisho.

Unaweza kutumia maswali yaliyopendekezwa kutengeneza maswali yako mwenyewe ya utafiti wa watumiaji wa maudhui kwa ajili ya chombo chako cha habari au maalum kwa kipindi chako unachofanyia kazi. Zipo tovuti za kukusaidia kujenga muundo wako wa maswali ya utafiti kama vile Google Forms na SurveyMonkey. Tovuti hizi zinasaidia kusambaza maswali mtandaoni au kuchapisha nakala na kuzisambaza kwa wanajamii wako.

Zungumza pia na mhariri wako na watu wengine katika chombo chako cha habari kujua zaidi au hata kufanya kazi na wafanyakazi wenzako kufanya utafiti wa mtaaani katika eneo ambalo chombo chako kinalifikia au chapisha swali moja au mawili katika kurasa zako za mitandao ya kijamii.

Hii itasaidia pia kujenga picha nzuri ya watumiaji wako wa maudhui.

## 1.6 - Kutumia lugha sahihi kwa watumiaji wako wa maudhui

Moja ya changamoto zinazokukabili kama mwandishi wa habari katika kutoa taarifa za mabadiliko ya tabia nchi ni misamiati migumu. Maneno na maandishi kama ...

- **Mabadiliko ya tabia nchi ya kibinadamu** *maana* yake mabadiliko ya tabia nchi yanayo-sababishwa na shughuli za kibinadamu
- **Nishati anuwai** *maana* yake nishati inayotokana na vyanzo vinavyosindikika, vyanzo vya kibaolojia kama vile mazao ya mahindi na miwa na aina nyingine ya taka
- **Nyayo za gesi ukaa** *ikimaanisha* kiwango cha gesi ukaa inayozalishwa na mtu mmoja mmoja au shirika katika kipindi fulani au kiwango cha gesi ukaa kilichozalishwa wakati wa kuzalisha bidhaa fulani
- **Kuongezeka kwa kemikali baharini** *ikimaanisha* neno linalotumika kuelezea mabadiliko ya kemikali katika ulimwengu wa bahari. Kwa uchache robo ya gesi ukaa inayozalishwa, inanyonywa na bahari na hivyo kufanya maji ya bahari kuwa na kemikali nyingi. Hii inaweza kuathiri viumbe bahari, kuua matumbawe na kuathiri wanajamii wanaotegemea bahari kwa ajili ya uvuvi

Mifano hiyo hapo juu inatoka katika kamusi ya Mabadiliko ya tabia nchi ya BBC. Kiunganishi katika kamusi hiyo na nyingine zinazofanana vinaweza kupatikana mwishoni mwa sehemu hii.

Hatua ya kwanza ya kuzuia matumizi ya misamiati migumu ni kuweza kuifahamu. Iwe unazungumza kwa lugha ya Kiswahili, Kingereza au lahaja (dialect) za kimkoa (makabila) usitumie maneno au sentensi ambazo huzielewi kwasababu upo uwezekano mkubwa kuwa hata watumiaji wako wa maudhui pia hawataelewa. Tumia lugha ambayo mtumiaji wako wa maudhui anaielewa ili kuifanya habari yako iwe na maana na hivyo kukuza uelewa.

### Mfano: Mabadiliko ya tabianchi kuanzia Mwanzo

**Evalilian Massawe** mbaye ni mtangazaji wa redio katika Shirika la Utangazaji Tanzania (Tan-zania Broadcasting Corporation -TBC) alimhoji mtaalam wa mabadiliko ya tabianchi ili kupata maelezo ya msingi. Kipindi kinajulikana kama Mabadiliko ya TabiaNchi Tangu Mwanzo, na ni mfululizo wa vipindi vyake vijulikanavyo kama Hadithi za Mazingira (Eco Tales). Kipindi hicho kinahabarisha wasikilizaji ni kwa namna gani shughuli zao za kila siku zinachangia katika mabadiliko ya tabia nchi.



*Evalilian Massawe*

Unaweza kukipata kipindi hicho hapa: https://creators.spotify.com/pod/profile/evalilian-massawe/episodes/CLIMATE-CHANGE-FROM-SCRATCH-e29n1hv

Evalilian pia ni mwanachama wa Mtandao wa Oxford wa Waandishi wa Habari za Mabadiliko ya Tabia Nchi, mpango wa Taasisi ya Reuters ya Mafunzo ya Uandishi wa Habari katika Chuo Kikuu cha Oxford nchini Uingereza, programu iliyoazishwa kusaidia waandishi wa habari duniani kote kuboresha ubora na uelewa wa mabadiliko ya tabia nchi. Ushauri wake ni kwamba wewe kama mwandishi jaribu kuzungumza na watumiaji wako wa maudhui katika njia ambayo inahusiana moja kwa moja na maisha yao.

*"Naamini ni jambo muhimu sana kutambua watumiaji wako wa maudhui ili kujua nini cha kuwapatia au ni lugha gani ya kutumia … nilikuwa naamini kuwa watu hawa hawavutiwi na masuala ya mabadiliko ya tabia nchi … nikafikiri, je ni jinsi gani naweza kukutana nao pale wanapoishi? Je ni jinsi gani naweza kuzungumzia suala la mabadiliko ya tabia nchi kana kwamba nazungumza nao moja kwa moja?"* (Evalilian Massawe)

## 1.7 – Changamoto

Zipo changamoto zinazowakabili waandishi wa habari wanaoandaa taarifa za mgogoro wa mabadiliko ya tabia nchi. Baadhi ya changamoto ni ngumu zaidi kuzikabili kuliko nyingine. Tutatazama kwa undani baadhi ya changamoto hizo ambazo unaweza kuzitambua:
- Nawezaje kutumia takwimu?
- Jinsi gani nawezakupata takwimu?
- Nawezaje kupata mtaalamu wa kunisaidia kusimulia hadithi yangu?
- Ni jinsi gani naweza kuwawajibisha walioko madarakani?
- Nini haki zangu za kisheria na wajibu wangu?
- Jinsi gani naweza kubakia salama?

### Jinsi gani naweza kutumia takwimu?

Takwimu ni njia yenye ufanisi Zaidi ya kuhakiki taarifa na kuelezea hadithi kwa njia tofauti. Lakini kutokana na mawazo kuwa takwimu 'ni ngumu mno' kuzipata na inaweza kuwa kikwazo cha kuzitafuta. Hivyo:
- Fikiria kuhusu kanzidata kama mhojiwa mwingine
- Iulize maswali yanayofanana na ambayo utamuuliza mwanadamu pia
- Hii inaweza kuwa njia yenye ufanisi mkubwa kuhakiki taarifa na kuelezea hadithi yako kwa njia tofauti

### Wapi naweza pata takwimu?

Hatua ya kwanza ni kujua wapi unaweza kupata takwimu. Kupata takwimu kunaweza kuwa changamoto kwani kunaweza kutegemea ni kwa kiwango gani serikali ya kitaifa na serikali za mitaa, mashirika ya afya na mazingira yako tayari kutoa takwimu hizo.

'Takwimu wazi' ni takwimu rasmi ambazo zimesambazwa kwenye intaneti. Tovuti ambazo unaweza kupata takwimu za Tanzania ni pamoja na:

- Africa Data Hub: https://www.africadatahub.org/
- Open Data Inception – 2600+ Open Data Portals Around the World: https://datahub.io/collections/climate-change
- World Bank: https://data.worldbank.org/country/tanzania

Yapo masomo zaidi ya jinsi ya kutumia takwimu katika kuelezea hadithi katika Sehemu ya 2.

**Wapi naweza pata wataalam kusaidia taarifa za habari yangu? (kutafuta vyanzo vya habari)**

Kuelewa misamiati ya kifedha, kisiasa na kisayansi pamoja na kutafsiri takwimu ni sehemu muhimu katika kuandika habari za mgogoro wa mabadiliko ya tabia nchi. Unaweza kuwa unaandikia katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabia nchi (COP) au unajaribu kutafsiri jinsi gani matokeo ya karibuni ya mada ya utafiti wa Umoja wa Mataifa yanaonyesha jinsi gani mabadiliko ya tabia nchi yanaathiri watumiaji wako wa maudhui. Ni muhimu kuwa sahihi na kuelewa misamiati midogo midogo, kwa mfano ahadi ya kupunguza gesi ukaa kwa kiwango cha chini iwezekanavyo na ahadi za kuondoa kabisa gesi ukaa.

Ufumbuzi hapa ni rahisi. **Omba msaada!**

- Tazama kwenye tovuti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi kupata taarifa za karibuni, takwimu na maandiko au wasiliana na ofisi yao ya habari moja kwa moja.
- Zungumza na kutengeneza uhusiano na wataalamu wa mabadiliko ya tabia nchi kutoka nchini Tanzania (katika vyuo vikuu, mashirika yasiyo ya kiserikali, vyombo vya serikali na taasisi za utafiti)
- Fuatilia waandishi wa mazingira na waliobobea kwenye masuala ya tabia nchi kwenye mitandao ya kijamii kujifunza mbinu zao

Ili kukusaidia kuanza, ipo orodha ya maeneo nchini Tanzania na nje ambapo unaweza kuji-unganisha na wataalamu wa masuala ya mabadiliko ya tabia nchi mwishoni mwa sehemu hii.

**Je ni jinsi gani unaweza kuwawajibisha wenye mamlaka?**

Kuandika habari za mazingira ni moja ya eneo hatari zaidi ambalo mwandishi anaweza kuliandikia. Mabadiliko ya tabia nchi ni sehemu ya eneo hilo. Sababu ya uhatari inaweza kufupishwa kwa maneno makuu matatu: siasa na fedha. Maslahi ya wanasiasa na wafanya-biashara (hususani wa kimataifa) vinaweza kufanya eneo hili kuwa hatari na gumu kuandika habari zinazohusu mabadiliko ya tabia nchi.

Kujua kuuliza maswali sahihi kufahamu ni nani aliyeketi katika kiti cha dereva: kuuliza KWA NINI jambo linatokea na NI NANI atafaidika, kunaweza kuwa eneo la kuanzia.

**Nini haki ya kisheria na wajibu?**

Ikiwa mwandishi utaandika habari za mabadiliko ya tabia nchi, sheria inaweza kufanya kazi kwa niaba yako au dhidi yako. Unaweza kutumia sheria za kitaifa au sheria za kimataifa kusaidia uchunguzi wako na kuwawajibisha wenye mamlaka. Lakini wenye mamlaka wanaweza na wanatumia sheria dhidi ya waandishi wa habari kujaribu kuwanyamazisha na kuwazuia kupata taarifa. Sehemu ya 4 itaorodhesha masuala muhimu na kusaidia kujua kuhusu haki yako ya kisheria na wajibu wako kama mwandishi wa habari.

**Nawezaje kubakia salama?**

Hii inaweza kuwa moja ya changamoto kubwa zaidi unazoweza kukabiliana nazo: kuhakikisha usalama wako wewe na chanzo chako cha habari. Ni dhahiri kwamba lipo swala la usalama wa kimwili na ule wa kidijitali na kuhakikisha kuwa una ulinzi wa kisheria. Kifungu cha 4 kitakupa mwongozo wa kina wa namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

## 1.8 - Zoezi: Dhoruba kali inasababisha mtafaruku

Fikilia kuwa uko katika mazingira haya halafu jibu maswali.

Mvua ya dhoruba inanyesha nchini Tanzania na kuua idadi kubwa ya watu na kuharibu mazao na makazi ya watu katika eneo unaloishi. Ukiwa kama mwandishi wa habari unatarajiwa kufanyia kazi habari hii na madhara ya dhoruba ya muda mrefu kwa siku kadhaa, wiki na hata miezi. Kwa kutumia kile ulichojifunza katika sehemu hii, soma maswali na kuamua jinsi gani unaweza kuandika habari hii. (Kwa toleo la pdf pekee: Majibu yanaweza kupatikana mwishoni mwa sehemu hii.  Zoezi hili litakuwa ni shirikishi katika jukwaa hilo).

**Swali 1**. Ni maswali gani ungeweza kuuliza kujaribu kujua kama hili ni suala la hali ya hewa au kama dhoruba hiyo ina uhusiano na mabadiliko ya tabia nchi? ***Dondoo***: Kuna zaidi ya jibu moja sahihi.

A. Je dhoruba hii inahusishwa na dhoruba zilizotokea kwa kuangalia kiasi cha mvua?
B. Ni kwa nini imejitokeza sasa?
C. Ni watu wangapi wameuawa au kukosa makazi kutokana na kuharibiwa na dhoruba?

**Swali la 2**. Ni nani unaweza kumuuliza kusaidia kupata majibu ya maswali hayo ili uweze kuandika kama dhoruba inahusiana na mabadiliko ya tabia nchi? ***Dondoo***: kuna majibu zaidi ya moja..

A. Akili mnemba
B. Mfanyakazi mwenzangu
C. Mwanasayansi wa masuala ya mabadiliko ya tabia nchi
D. Taasisi ya serikali
E. Mtu ambaye nyumba yake imeharibiwa na mafuriko

**Swali la 3.** Waandishi wenzako ambao wanaandika habari za michezo wanasema kuwa Habari hii siyo ya kuandikwa na watu wa michezo kutokana na dhoruba kuwa na uhusiano na mabadiliko ya tabia nchi. Je ni sahihi?

A. Ndiyo
B. Hapana

**Swali la 4.** Unaona taarifa katika shirika la Umoja wa Mataifa inatoa angalizo la kutokea kwa dhoruba nyingine kali zaidi nchini Tanzania ambayo wanaihusisha na mabadiliko ya tabia nchi. Ripoti inatumia maneno ya kifupisho kama *NDCs, adaptation, and mitigation bila kuelezea maana yake*. Je utafanya nini?

NDCs - Ufupisho wa National Determined Contributions: ni mipango kazi ya nchi wanachama ya kukabiliana na gesi ukaa na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.
Adaptation - kufanya Maandalizi ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ya wakati husika kama kujenga uzio kuzuia mafuriko au kupanda mazao yanayostahimili ukame
Mitigation - Kuchukua hatua za kukabiliana na gesi ukaa ili kuzuia ongezeko la joto duniani. Hatua hizo zinaweza kuwa kutumia nishati safi na salama kwa ajili ya kupikia n.k

A. Utarudia maneno na vifupisho vyake lakini utaelezea maana yake katika habari yako
B. Utarudia maneno na vifupisho vyake bila kuelezea zaidi katika habari yako
C. Utapuuza kabisa maneno na vifupisho vyake

## 1.9 - Mambo muhimu ya kuondoka nayo

Umefikia mwisho wa sehemu hii. Hapa unakumbushwa mambo muhimu matatu ambayo umejifunza.

**Jambo la kuondoka nalo 1:** Kuandika masuala ya mabadiliko ya tabia nchi ni kazi ya kila mwandishi wa Habari
**Jambo la kuondoka nalo 2:** Usitumie misamiati migumu na elezea habari kwa lugha ambayo watumiaji wako wa maudhui wanaielewa
**Jambo la kuondoka nalo 3:** Pata ushauri wa mtaalamu kukusaidia habari zako kuwa sahihi na zisizoegemea upande mmoja

## Vyanzo vya taarifa:

### Kwa ujumla

- Wasifu wa Uhimilivu Dhidi ya Ukame - Tanzania: https://www.ciwaprogram.org/wp-content/uploads/SADRI_Drought_Resilience_Profile_Tanzania.pdf
- Shirika la Utabiri wa Hali ya Hewa Duniani: https://wmo.int/news/media-centre/extreme-weather-and-climate-change-impacts-hit-africa-hard
- IPCC: https://www.ipcc.ch/
- BBC Climate Change Glossary: https://www.bbc.co.uk/news/science-environment-11833685

### Tanzania: Sera za mabadiliko ya tabia nchi

- Mkakati wa Taifa wa Tanzania wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi wa mwaka 2021-2026: https://www.ncmc.go.tz/wp-content/uploads//2022/10/National-Climate-Change-Response-Strategy.pdf
- Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi 2025–2035: https://unfccc.int/sites/default/files/resource/NAP_UNITED%20REPUBLIC%20OF%20TANZANIA.pdf
- Dira ya 2050: Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: https://www.planning.go.tz/uploads/documents/en-1752762713-THE%20TANZANIA%20DEVELOPMENT%20VISION%202050.pdf
- Mtandao wa Utekelezaji wa Hatua za Tabia Nchi: https://cantz.or.tz/programmes

### Tanzania: Sheria

- Kituo cha Kimataifa cha Sheria za Mashirika yasiyo ya Kibiashara: https://www.icnl.org/wp-content/uploads/Tanzania-Understanding-Your-Right-to-Information.pdf
- Tanzania Media Laws: A handbook for practitioners: https://www.icnl.org/wp-content/uploads/Tanzania-practical-manual-final-with-FHI360-covers.pdf

### Tafuta mtaalam wa kukusaidia:

- Mtandao wa Utekelezaji wa Hatua za Tabianchi Tanzania ( unajumuisha asasi za kiraia kutoka zaidi ya nchi 130 ukilenga kushawishi kupunguza gesi ukaa na kuimarisha hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi): https://cantz.or.tz/who
- CLARE Climate Adaptation and Resilience: https://clareprogramme.org/clare_countries/tanzania/
- Climate-U Transforming Universities for a Changing Climate: https://www.climate-uni.com/tanzania-team
- Vituo vya Rasimali Asilia na Maendeleo: https://cnrd.info/cnrd-network-partner/institute-for-environment-and-development-sustainability/
- Taasisi ya Mazingira na Maendeleo Endelevu: https://www.ieds.or.tz/index.php/about-us/
- Wataalamu wa Mabadiliko ya Tabia Nchi Barani Afrika (UNECA): https://uneca.org/african-climate-policy-centre/african-climate-change-experts
- Mamlaka ya Utabiri wa Hali ya Hewa Tanzania: https://www.meteo.go.tz/

## Majibu ya mazoezi

**1.3** Jibu sahihi ni c, au yote mawili. Mafuriko ni sehemu ya kawaida ya mfumo anuwai. Mito kufurika mara kwa mara na mvua kubwa ni sehemu ya mzunguko wa hali ya hewa. Inatokea wakati mvuke unapopanda juu kutengeneza mawingu ambayo baadaye yanashusha mvua. Hata hivyo, kama mvua kubwa inajitokeza mara kwa mara, na inanyesha kwa vipindi virefu, hiyo inaweza kuhusishwa na mabadiliko ya tabia nchi. Hewa ya mvuke inaweza kubeba unyevu mwingi zaidi, na kusababisha mvua kubwa.

**1.8** - **Dhoruba yasababisha mtafaruku**

**Swali 1.** Majibu ni a na b. Kujua idadi ya watu waliouawa au kuharibiwa kwa makazi yao ni sehemu muhimu ya habari lakini haiwezi kuelezea kama dhoruba hiyo inahusiana na mabadiliko ya tabia nchi. Hata hivyo, kama dhoruba zinahusishwa na mabadiliko ya tabia nchi, idadi ya watu waliokufa au kuharibiwa makazi yao inaonyesha madhara ya kimaangamizi ambayo mabadiliko ya tabia nchi yanasababisha katika jamii yako.

**Swali 2**. Majibu sahihi ni c na d. Kujua kama kuna uhusiano kati ya dhoruba na dhoruba unapaswa kuongea na mtaalam kama vile mwanasayansi wa mabadiliko ya tabia nchi. Mtu ambaye makazi yake yameharibiwa anafaa kuongea kuonyesha uhusiano wa madhara ya mabadiliko ya tabia nchi kwa watumiaji wako wa maudhui (tutaangalia katika usimuliaji wa hadithi katika Sehemu ya 3) lakini siyo wataalam wa mabadiliko ya tabia nchi wala waandishi wenzako. Kuhusu akili mnemba (AI bot), haiwezi kutegemewa kutoa taarifa sahihi.

**Swali la 3**. Jibu sahihi ni b. Viwanja vya michezo vilivyojaa maji ya mafuriko vinaweza kuwa taarifa unazoweza kuingiza katika habari yako lakini pia ni habari inayofaa kwa mwandishi wa habari za michezo. Nini madhara katika uwanja wa mazoezi au mashindano? Nani atasafisha viwanja na ni nani atalipia gharama? Kuna maswali mengi ambayo mwandishi wa habari za michezo anaweza kuuliza kufanya habari ya mabadiliko ya tabia nchi kuwafaa watumiaji wake wa maudhui na kuwapatia uwezo kuuliza maswali sahihi kwa wenye mamlaka ambao wanaweza kutoa baadhi ya majibu.

**Swali 4**. Jibu sahihi ni a. Ripoti inatumia misamiati na ni kazi yako kuelezea misamiati hiyo kwa watumiaji wako wa maudhui. Kupuuzia maneno na vifupisho haitawasaidia watumiaji wako wa maudhui kuelewa mada ya mabadiliko ya tabia nchi.

# Sehemu ya 2 - Usimualiaji wa Hadithi: Kuifanya hadhira ijali kuhusu mabadiliko ya Tabia Nchi

### 2.1 – Je simulizi ni ipi?

Je ni simulizi gani mpya na ya kusisimua uliyosoma, uliyoangalia au kusikiliza mara ya mwisho na ambayo ilikufanya utafakari kwamba natamani ningefanya hivyo. Haiyamkini simulizi iliyoteka ufahamu wako ilijumisha baadhi ya vitu ambavyo tunakwenda kuangazia katika kifungu hiki- vitu ambavyo vinaweza kusaidia simulizi za habari ziwe hai na kuhusisha hadhira.

Waandishi wa habari ni wasimuliaji wa stori lakini inaweza kuwa ngumu kusimulia simulizi za mabadiliko ya tabia nchi kwa wahariri, labda kwasababu ya mtizamo wa hadhira ambao mara nyingi hupimwa kwa kutegemea taarifa zenye mashamsham au zilizotoka hapo punde, zenye figisu za kisiasa, tishio la kiafya, au mafanikio kwenye michezo. Je unawezaje kuifanya hadhira na wahariri kujali? Hili ndilo swali tutakalokuwa tunajaribu kulijibu kwenye kifungu hiki.

### 2.2 – Kuweka wazi uhusiano na mabadiliko ya hali ya hewa

Ni vema ukafanya maandalizi kidogo ya kuangazia mambo muhimu kabla ya kuanza kazi ya kutoa simulizi. Kuuliza na kujibu maswali sahihi kutarahisisha kadri unavyokwenda. Cha muhimu zaidi ni kwamba kuuliza maswali sahihi kutakusaidia kuweka wazi uhusiano na mabadiliko ya tabianchi hata kama hauonekani wazi mara moja.

**Mathalani**: Simulizi hii iliyoandikwa vema na mwandishi wa habari Jeniffer Gilla inafichua uhusiano kati ya ongezeko la Ukatili wa Kijinsia dhidi ya wanawake wa Kimaasai na madhara ya mabadiliko ya tabia nchi duniani. Ukame na upungufu wa maji vinawalazimisha wanawake hawa kwenda mbali kutafuta maji na malisho ya mifugo. Kutumia muda mrefu mbali na nyumbani huweza kupelekea vipigo kutoka kwa waume zao. Simulizi hii inapanua zaidi mawanda ya uelewa kutoka kwenye mtazamo wa kijiji, kwenda kwenye ule wa kikanda, kitaifa na kimataifa na kutoa suluhisho la kuboresha hali zao. Bofya hapa ili kupata simulizi hiyo: https://habitatmedia.co.tz/maasai-women-see-increased-gbv-as-climate-change-affects-their-livelihoods



Hapo chini ni orodha ya maswali unayoweza kutumia ili kuonyesha uhusiano unaoweza kuwepo kati ya simulizi yako na mabadiliko ya tabianchi.

- **Ni maswali gani niulize?**

Chukulia mfano huu: *Umegundua kwamba polisi wanachunguza kiwanda cha nguo kilichoko kwenye mji ambao unaaminika kuwa kitovu cha mtandao wa usafirishaji haramu wa binadamu.* Mwanzoni hakuonekani kuwa na uhusiano wowote na mabadiliko ya tabianchi- je utaanzaje kuibua? Chukua dakika chache kutafakari utafanya nini na kisha soma baadhi ya mapendekezo hapo chini:

Uliza:
- *Je ni nani anasafirishwa?* Mathalani, kuulizia wanakotoka kunaweza kuweka bayana iwapo wamelazimika kutoka kwenye nchi ambayo imeathirika vibaya na ukame au mafuriko.
- *Kwanini wapo mjini?* Mathalani unaweza kugundua kwamba wao ni wahamiaji ambao ni wahanga wa maswala ya tabianchi na uchumi. Uchumi wao umeporomoka kutokana na mzunguko wa majanga ya ukame na mafuriko.
- *Ni kwanini walikuwa wanafanya kazi kiwandani?* Mathalani, mafuriko yenye madhara makubwa ya hivi karibuni yamewaacha watu wengi bila makazi na kuwafanya kuwa wahanga wa makundi ya kihalifu yaliyowaahidi ajira na makazi.

- **Je ni nani naweza kumwajibisha?**

Kazi ya mwandishi ni kuwajibisha mamlaka: Hapa nakukumbusha kuhusu ile hali? Umegundua kwamba polisi wanachunguza kiwanda cha nguo kilichoko kwenye mji wako ambao unaaminika kuwa ni kitovu cha mtandao wa usafirishaji haramu wa binadamu.

Ukiangazia zaidi unagundua kwamba makundi ya kihalifu ya wasafirishaji haramu wa binadamu yanaonekana kuhusika. Tafakari kwa dakika chache ili kuona unaweza kumwajibisha nani mwingine kisha soma baadhi ya mapendekezo hapo chini:

- *Uliza maswali kuhusu fedha*: Nani anapata fedha kutokana na hili? Je mtandao una ukubwa wa kiasi gani? Je ni kundi moja la wasafirishaji haramu au yapo makundi mengine ya kitaifa au wafanya biashara wa kimataifa na wanasiasa nyuma yake ambao nao wanafaidika?
- *Uliza maswali kuhusu masuala ya kisiasa*: Mathalani, je mwitikio wa kisiasa kuhusu ukame na mafuriko umekuaje? Je mkoa uliahidiwa rasilimali lakini hazikutolewa mapema kama ilivyotakiwa?

**Kuwa makini:** Kama ilivyobainishwa hapo awali, kuuliza maswali kunaweza kukuweka hatarini wewe na vyanzo vyako vya taarifa. Suala la usalama linaangaziwa zaidi kwa kina katika kifungu cha 4.

- **Vyanzo vyangu vya taarifa ni vipi?**

Kupata vyanzo sahihi: watu wa kuongea nao na sehemu ya kupata taarifa ni kitu muhimu katika usimuliaji mzuri wa hadithi. Ifuatayo ni kumbukizi ya suala hilo tena:
Umebaini kwamba polisi wanachunguza kiwanda cha nguo kilichoko kwenye mji karibu yako ambao unaaminika kuwa ni kitovu cha mtandao wa usafirishaji haramu wa binadamu.

Jipe dakika chache kutafakari ni nani utaongea nae na watu ambao wanahusiana moja kwa moja na simulizi kama polisi na wahanga wa biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu ambao unaweza kukutana nao:
- *Mtaalamu wa Mabadiliko ya tabia nchi*. Kuweka wazi uhusiano kati ya mabadiliko ya tabi-anchi unaweza kumaanisha kuhusisha wahojiwa ambao hawakutarajiwa. Wanaweza pia kutoa mtizamo mwingine, mpya na wa kuvutia.
- *Mwanasheria*. Je unahitaji ushauri wa kisheria kwa ajili ya simulizi yako? Vyombo vingi vya habari vina wanasheria japo yapo mashirika ambayo hutoa ushauri wa kisheria kwa waandishi wa habari nchiini Tanzania. Viunganishi kuhusu hilo vipo mwisho wa kifungu na taarifa zaidi zinapatikana katika kifungu cha 4.
- *Vyanzo vya Mtandaoni* (pata viunganishi mwisho wa kila kifungu) ili kukusaidia kuieleza hadhira yako juu ya majibu ya sayansi na sera.

Tutarejea kwenye vyanzo hapo baadae kwenye kifungu hiki.

- **Je nawezaje kuijengea uwezo hadhira yangu?**

Simulizi bora ya waandishi wa habari hujenga uwezo wa hadhira. Huiwezesha hadhira kuwa na fikra tunduizi kuhusiana na maamuzi yao na kuelewa maamuzi yanayofanywa na wenye mamlaka na namna ambavyo yanawaathiri. Hutoa taarifa ya namna ambavyo wanaweza kuwawajibisha walioko madarakani. Iwapo wewe kama mwandishi unaweza kufanya hilo litokee kwa kuwashirikisha kwenye simulizi inayohusiana na maisha yao- wewe ndie mtu ambae hadhira inamtafuta.



**Sylivester Domasa** ni meneja wa huduma za habari za kidijitali kwenye Kampuni ya Magazeti ya Serikali. Vilevile ni mwandishi mzoefu wa sayansi na mazingira. Anasema japo ni muhimu kwa waandishi wa habari kuuliza maswali ya muhimu kama nani, nini, lini, wapi, kwanini na namna gani, wanahitaji pia kuuliza maswali ya kina zaidi pale wanapokabiliana na simulizi inayojumuisha hadhira.

"*Nilipokuwa nafanya kazi magazetini nilikuwa nakimbilia kuuliza maswali kwa kuzingatia W tano na H. Kwa sasa sishughuliki sana na hilo. Ninachoangalia ni kama habari inajibu swali la kwa hiyo? Je hiki ndicho watu walioko mtandaoni wanakiangalia? Kwa hiyo kusimulia hadithi ni uwezo wa kujibu kitu ambacho mtu ataona kinamhusu*." (Sylivester Domasa)

Hoja kuu za **Sylivester**:

- Sylivester anasema swali muhimu ambalo waandishi wa habari wanapaswa kuuliza wanapochunguza simulizi ni kwa hiyo? Tafakari kipi kinaifanya simulizi kuwa ya muhimu na kwanini ina umuhimu kwa hadhira
- Simulizi inaweza kuwa ya mafanikio au anguko- cha muhimu ni kutoa kitu ambacho watu wanaweza kubeba uhusika.

Je unaitekaje hadhira yako? Hiki ndicho tutakachoangazia baada ya hapa.

### 2.3 - Dondoo muhimu za kutoa simulizi

Hizi ndizo dondoo muhimu za kutoa simulizi:
- Ipe simulizi sura ya kibinadamu
- Sauti zisizosikika
- Picha na Sauti
- Takwimu
- Uandishi unaojenga

Hebu tuangazie kwa kina kila dondoo.

- **Ipe simulizi sura ya kibinadamu**

Kuipa simulizi jina na kuweka sura kunaweza kuifanya kuwa ya kuvutia zaidi. Inaweza kusaidia kufanya masuala magumu ya sayansi kuwa muhimu kwa muktadha ambapo hadhira inaweza kubeba uhusika. Kuipa simulizi sura ya kibinadamu kwa kutumia visa mkasa kunaweza kutambulisha mtizamo wa mabadiliko ya tabia nchi na kutoa taswira ya utu. Iwapo watu watajiweka kwenye uhusika wa simulizi ni dhahiri kuwa watabaki nayo.

**Mathalani:** Zaidi ya watu 150 wamekufa kutokana na mafuriko na maporomoko ya udongo katika sehemu mbalimbali nchini mwezi Aprili 2024[1]. Maelfu ya watu waliachwa bila makazi. Janga kama hili linaweza kuwa zito kwa hadhira licha ya waandishi kuripotia.

[1] https://reliefweb.int/disaster/fl-2024-000058-tza

Mfano huu unaanza na madhara ya uharibifu unaotokana kwa wahanga wawili wa mafuriko. Mahojiano yanaweza kufanyika kutoka mbali kama hali katika eneo husika ni hatari. Bofya kiunganishi hiki kupata simulizi: https://www.thecitizen.co.tz/tanzania/news/national/rufiji-floods-voices-of-resilience-amidst-devastation-4588450

- **Sauti zinazokosekana**

Swali moja la muhimu la kuuliza ni: Ni sauti zipi zinakosekana? Chunguza kwa dhati simulizi zako:
- Je ni watu wangapi ulioongea nao walikuwa wanaume au Wanawake?
- Wangapi walikuwa wanataaluma? Mf. Wanasiasa, mwanasheria au kiongozi/afisa
- Je ni wangapi walikuwa watu wa kawaida ambao waliathirika na simulizi hiyo?

Ina umuhimu kwa maana mbili:

***Kwenye eneo husika:***
- Sauti na mitizamo mipya inaweza kuifanya simulizi yako kuwa ya kuvutia zaidi na ya kipekee
- Utakuwa hujatenda haki kwa hadhira yako iwapo utawapuuza watu fulani
- Iwapo idadi ya wasikilizaji/wasomaji/watazamaji itashuka inaweza kuathiri moja kwa moja kazi yako

***Katika kiwango cha juu zaidi:***
- Watu wanaohisi kupuuzwa watakwenda popote kutafuta habari jambo linaloweza kusababisha kusambaa kwa taarifa potofu na za uongo
- Iwapo mathalani watoto, wanawake na makundi maalumu kama watu wenye ulemavu hawatajumuishwa kwenye mazungumzo, inamaanisha simulizi itakuwa haijafanyika jambo linaloweza kuathiri mabadiliko ya sera yanayofanywa na Serikali
- Usimuliaji wa simulizi unaovutia unaweza pia kuifanya mada kuwa muhimu zaidi kwa hadhira ya kitaifa na kimataifa, kwani watavaa uhusika zaidi pale wanapojiona katika maisha ya watu wa kawaida

**Mathalani**: Sauti za Watoto zilipewa umuhimu mkubwa kwenye simulizi hii ya Wangu Kanuri ambae alisafiri kwa siku mbili ili kushuhudia namna mabadiliko ya tabia nchi yanavyoathiri maisha ya watoto na walimu katika shule kijijini Kenya. Hadithi zao zilisimuliwa kwa umahiri mkubwa katika simulizi nzima. Pata simulizi hapa: https://nation.africa/kenya/health/classrooms-or-ovens-the-price-of-schooling-under-a-scorching-sun-5097434

- **Picha**

Picha nzuri ni rahisi na ina uwezo mkubwa wa kuiteka hadhira.

**Mathalani**: Angalia picha hizi mbili ambazo zote zimetumika kuonyesha taswira ya simulizi moja.  Ni ipi ungependa kuisoma?

Kuchagua picha sahihi kunaweza kuwa jambo la mtazamo binafsi, lakini fikiria picha nzuri kama dirisha la hadithi yako – iwapo watu wataipenda, wataingia ndani. Kwa mantiki hii, kumuonyesha mtu kwenye picha kunaweza kusaidia kutengeneza uhusika wa kihisia.  Chupa ya plastiki pekee inaweza kuwa popote.





Vilevile tafakari namna ambavyo picha inaweza kujenga uhusiano na hadhira. Mfano haitakuwa na mantiki iwapo picha unayotumia itakuwa ya dubu barafu (polar bear) iwapo unajaribu kuelezea madhara ya mabadiliko ya tabianchi kwa watu wanaoishi mkoa wa Mbeya.

- **Mlio/Sauti**

Sauti ina nguvu kubwa ya kumfanya mwandishi kujenga uhusiano na hadhira (wasikilizaji) katika namna ambayo ni ya kipekee. Wewe ni sauti inayoaminika kwenye masikio yao. Watu wengi nchiini Tanzania bado wanategemea redio ili kupata taarifa lakini bado wanahitaji sababu ya kufungulia redio hizo. Redio inayotoa simulizi bora huwapa wasikilizaji hisia za kujiona wako pamoja nawe na kuwaunganisha kwa kuchora taswira kupitia sauti.

**Mathalani**: Kuanzia kwenye sauti za wadudu hadi kwa watu wanaotembea kwenye tope linalosikika, Redio ya kimataifa ya Farm huwapeleka wasikilizaji hadi kwenye maisha ya jamii za wakulima barani kote.

Katika moja ya mifano, wakulima nchiini Ghana walielezea namna ambavyo wamekuwa wakitengeneza mbolea yao ya mboji ili kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Programu hiyo imetengenezwa kwa mfumo wa video fupi yaani reel kwa ajili ya mitandao ya kijamii ambapo unaweza kusikiliza kupitia kiunganishi hiki: https://www.youtube.com/shorts/yMNgU_gfnJw

Unaweza pia kupata mifano zaidi kutoka Redio ya Kimataifa ya Farm hapa: https://www.youtube.com/@FarmRadioInt/featured

- **Takwimu**

Takwimu ni moja ya chanzo chako kingine cha simulizi and inapokuja kwenye kuthibitisha ukweli, masuala yanayohitaji kuthibitisha ni yale yale:

- Je unahitaji ruhusa ili kutumia?
- Je kuna masuala ya kisheria ya kuzingatia Mf. Je takwimu/taarifa zinajumuisha taarifa binafsi kama majina ambavyo vinatakiwa kubaki siri?
- Je taarifa/takwimu ni sahihi? Je zinatoka kwenye chanzo cha uhakika?

Sayansi ya tabianchi ina utajiri wa takwimu/taarifa: kuanzia kwenye usafiri hadi matumizi ya nishati na zaidi na hivyo kuifanya kuwa rasilimali kubwa kwa waandishi. Kazi yako ni kuiongoza hadhira kupitia takwimu. Je zinatoa simulizi gani?

**Mathalani**: Uchunguzi wa kina uliojulikana kama 'kunyonywa na kuachwa wakavu' ulifanywa na shirika la InfoNile ambapo lilitumia takwimu kuweka wazi kiwango cha uporaji wa ardhi kinachofanywa na wawekezaji wa kigeni na wazawa ambapo ilidaiwa kuwa si tu unaziacha jamii za wazawa bila makazi, lakini pia unaharibu rasilimali za asili katika nchi za Uganda, Sudan, Ethiopia na Misri. Pata simulizi hapa: https://infonile.org/sucked-dry/


Utapata viunganishi vya baadhi ya takwimu na nyenzo mwishoni mwa kifungu hiki.

- **Uandishi wa habari unaojenga**

Vichwa vya habari vyenye riwaya za kubuniwa na zenye vitisho kuhusu mabadiliko ya tabianchi vinaweza kuvutia hadhira, lakini vinaweza pia kuwa na madhara. Vinaweza kuacha watu wakihisi kutoweza kufanya chochote na kukata tamaa. Simulizi hasi hazipaswi kupuuzwa, lakini njia mojawapo ya kuvutia hadhira ni kutoa kitu cha kujenga badala ya kuonyesha matatizo pekee.

Wakati mwingine sio rahisi kupata mwanzo wa simulizi wenye kujenga- suluhisho ni kuuliza swali nini kinafuata? Moja kwa moja huangazia siku za usoni na kutoa njia zinazojumuisha suluhisho la kisayansi ndani ya simulizi.

**Mathalani**: Rasilimali maji zina shinikizo kubwa kutokana na ukame. Simulizi hii inaweka wazi namna vijiji 12 vilivyofanya kazi kwa pamoja na kujenga mabwawa na hifadhi ili kupunguza upungufu wa maji. Pata simulizi hapa https://www.ipsnews.net/2024/07/climate-smart-strategies-revitalized-tanzanias-livestock-sector/



## 2.4 – Kuifanya simulizi yako kuwa sehemu ya riwaya duniani

Mabadiliko ya tabia nchi ni suala la kidunia.  Ili kutoa simulizi yote unahitaji kuhakikisha kuwa simulizi yako ya hapo ulipo inaunda taswira kubwa zaidi. Ni aina ya usimuliaji wa riwaya unaoweza kuinufaisha taaluma yako. Iwapo utatengeneza simulizi ambayo itahusisha Jamii, kitaifa na kimataifa, utavutia hadhira mpya.

**Mathalani:** Ripoti hii inawaleta pamoja wakulima, wabunifu wa akili mnemba (AI) na viongozi wa Jamii ili kuangazia namna AI inavyosaidia kupambana na changamoto za mazao. Ripoti inachangia kwanye swala zito la kidunia la namna teknolojia inavyoweza kusaidia maendeleo endelevu. Pata simulizi hapa: [https://necjogha.net/smarter-skies-how-tanzanian-innovators-are-using-ai-for-climate-action/](https://necjogha.net/smarter-skies-how-tanzanian-innovators-are-using-ai-for-climate-action/)




Dondoo za kuunganisha simulizi na mjadala wa mabadiliko ya tabia nchi duniani na kinyume chake:- -

- Chukulia kwamba hakuna kitu kinachoitwa simulizi ya eneo husika ya mabadiliko ya tabia nchi
- Tafuta ulinganifu wa kile kinachotokea hapo ulipo na kile kinachotokea katika eneo lingine. Inasaidia hadhira kutambua kwamba hawako peke yao
- Hadhira ya eneo husika watataka kujua madhara kwenye maisha yao ya kila siku lakini hadhira ya kitaifa na kimataifa itashiriki iwapo utaelezea madhara kwao kwenye bei za chakula mathalani, kukosekana kwa mavuno

## 2.5 - Zoezi: Polisi wavamia kiwanda cha nguo

Ngoja turudi kwenye mifano ya mwanzo wa kifungu hiki. Simulizi sasa imekwenda mbali zaidi.

*Polisi wamevamia kiwanda cha nguo kwenye mji ulioko na wanachunguza tuhuma za mahusiano kati ya kiwanda hicho na mtandao wa usafirishaji haramu wa binadamu. Vyanzo vinakujuza kuwa wafanyakazi kwenye kiwanda hicho ambao walikuwa wananyonywa na walilazimika kuondoka katika sehemu ya nchi ambayo ilikuwa inakabiliwa na ukame mkali uliofuatiwa na mafuriko na kuleta maafa makubwa. Unagundua pia kwamba kiwanda kilikuwa kinazalisha nguo za bei ndogo kwa ajili ya kusambaza nchi za nje.*

Tafakari namna ambavyo utasimulia simulizi hii kwa kujibu maswali. Utapata majibu mwishoni mwa sura hii.

**Swali la 1**. Je kuna mtazamo wa mabadiliko ya tabianchi katika hadithi hii?

A. Ndiyo
B. Hapana
C. Labda

**Swali la 2**. Je ni maswali gani ambayo utajaribu kuuliza ili kuweka wazi sababu za kisiasa na kiuchumi katika simulizi yako ili kumuwajibisha mtu? Kidokezo: Lipo jibu zaidi ya moja

A. Uliza nani anamiliki kiwanda
B. Uliza nani mwingine ambae amewekeza kifedha katika kiwanda hicho
C. Uliza watu wangapi walikutwa wanafanya kazi kwenye kiwanda
D. Uliza mamlaka zilikuwa na mwitikio gani katika ukame wa awali na mafuriko na kama ahadi zilitolewa na/au hazikutekelezwa

**Zingatia**: Kama ilivyobainishwa hapo mwanzo, a maswali haya yanaweza kuwa hatari kwa waandishi wa habari na vyanzo vyao. Unaweza kupata ushauri jinsi ya kuwa salama kwenye sehemu ya 4.

**Swali la 3**. Je ni namna ipi ingekuwa ya kuvutia zaidi ya kuibua ubinadamu katika simulizi hii?

A. Kumhoji mwanasanyansi wa mazingira
B. Kumhoji mwanasiasa katika eneo husika
C. Kumhoji afisa wa polisi ambae alihusika na uvamizi
D. Kumhoji mmoja wa wafanyakazi aliesafirishwa kiharamu

**Swali la 4**. Je unawezaje kuifanya simulizi kuwa yenye mvuto kwa hadhira ya kitaifa na kimataifa?

A. Weka wazi uhusiano kati ya mabadiliko ya tabia nchi na duka la nguo za bei rahisi
B. Mhoji mwanasayansi wa mabadiliko ya tabia nchi kuhusiana na taswira ya kidunia
C. Usifanye chochote kwani ni stori ya eneo husika tu

### 2.6 - Mambo muhimu ya kuzingatia

Umefika mwisho wa kifungu hiki.  Yafuatayo ni mambo matatu muhimu ambayo umejifunza:

**Jambo muhimu la kuzingatia la 1**: Uliza maswali sahihi:
- Weka wazi mahusiano na mabadiliko ya tabia nchi
- Chagiza uwajibikaji
- Jengea uwezo hadhira

**Jambo muhimu la kuzingatia la 2**: Jumuisha sauti zinazokosekana ili kuzifanya simulizi zako kuwa za mvuto, za kipekee na muhimu kwa hadhira yako

**Jambo muhimu la kuzingatia la 3**:  Tengeneza simulizi zinazoweza kuleta mabadiliko ya tabia nchi ya kidunia au kuifanya picha ya kidunia iwe na mahusiano na ile ya kijamii

### Vyanzo vya jumla

Kozi ya bure ya masomo ya mtandaoni ya Thomson Foundation:

- Simulizi za kiafrika: Mwongozo kwa waandishi wa habari wa namna ya kusimulia hadithi nzuri zaidi kuhusu Afrika - https://www.journalismnow.org/course/african-stories-a-guide-for-journalists-on-how-to-tell-better-stories-about-africa
- Kuandika Habari- Sanaa ya kusimulia hadithi - https://www.journalismnow.org/course/news-writing-the-art-of-storytelling
- Uandishi wa kipekee: Sanaa ya kusimulia hadithi - https://www.journalismnow.org/course/advanced-writing-the-art-of-storytelling
- Uchambuzi wa Habari: Sanaa ya Kusimulia hadithi - https://www.journalismnow.org/course/news-analysis-the-art-of-storytelling
- (Usimuliaji wa hadithi kwa kutumia sauti) utoaji wa vipindi vya sauti mtandaoni: kutengeneza - https://www.journalismnow.org/course/podcasting-making-it

- Africa Data Hub: https://www.africadatahub.org/
- DataJournalism.com: https://datajournalism.com/
- Solutions Journalism Network: https://www.solutionsjournalism.org/
- Code of ethics for media professionals  - Media Council of Tanzania: https://mct.or.tz/wp-content/uploads/2023/12/Code-of-ethics-2020.pdf

## Majibu ya mazoezi

### 2.5 - Polisi wavamia kiwanda cha nguo

**Swali la 1**. Jibu bora labda ni C. Ukame na mafuriko ni sehemu ya mifumo ya hali ya hewa, Hivyo unatakiwa kujua kama matukio haya hutokea mara kwa mara na kwa ukubwa na kama matokeo yake yanahusiana na mabadiliko ya tabia nchi. Rejea kifungu cha 1 iwapo unahitaji kufanya hivyo ili kujikumbusha.

**Swali la 2**. Majibu bora zaidi ni a, b na d. Kufuatilia masuala ya fedha ni sehemu muhimu ya uandishi wa habari za mazingira za kiuchunguzi hivyo basi kujua nani anamiliki kiwanda na majina ya wawekezaji ni sehemu muhimu ya kuanzia. Kuulizia mwitikio wa mamlaka kunaweza kubainisha makosa, uzembe au rushwa kwa upande wa watendaji kama waliahidi kutoa ulinzi dhidi ya mafuriko au msaada kwa wakulima mathlani na hayo hayakutokea. Kuuliza ni watu wangapi walikutwa kiwandani wanafanya kazi ni swala muhimu lakini halisaidia kumwajibisha yoyote.

**Swali la 3**. Jibu bora ni d, mhoji mmoja wa wafanyakazi waliosafirishwa. Wahojiwa wote waliopendekezwa ni muhimu kwa simulizi yako lakini stori ya mfanyakazi inaweza kuwa ndiyo bora zaidi ya kuanzia. Iwapo umeongea na mfanyakazi, unahitaji kumpa muda wa mahojiano. Anaweza kuwa ana majeraha kisaikolojia na anawezakutaka asitajwe. Ni mahojiano ambayo yanatakiwa kufanyika kwa uangalifu mkubwa na kupangwa mapema.

**Swali la 4**. Jibu zuri zaidi hapa ni kuweka bayana mahusiano kati ya madhara ya mabadiliko ya tabia nchi na maduka ya nguo za bei nafuu. Shirika la Umoja wa Mataifa linaitaja sekta ya mitindo kama moja ya sekta zinazochafua zaidi duniani, ikihusika na hadi asilimia nane ya uzalishaji wa gesi chafuzi za anga[2]. Hii inahusiana moja kwa moja na simulizi za walaji duniani kote. Mahojiano na mwanayasayansi wa tabia nchi ni muhimu kwa simulizi yako lakini mahojiano kuhusiana na hali ya kidunia siyo ya kipekee kwa simulizi yako wala si ya kusisimua. Kutofanya kitu kama ilivyoainishwa, hakutakiwi kuwa sehemu ya chaguo lako.

[2] https://news.un.org/en/story/2025/03/1161636

# Sehemu ya 3 – Upotoshaji kuhusu tabianchi: Kuelimisha hadhira

## 3.1 - Kusambaa kwa taarifa potofu

Ripoti ya African Digital Democracy Observatory inadai kwamba, "*taarifa potofu zinaifanya Tanzania kuwa hatarini zaidi kukumbwa na mishtuko ya tabianchi. Watu wanapoamini madai ya uongo, wanachelewa kuchukua hatua ambazo zingeweza kulinda mashamba yao, makazi yao na kipato chao.*"[1]

Taarifa potofu kuhusu mabadiliko ya tabianchi zimesambaa sana nchini Tanzania kama ilivyo katika sehemu nyingine nyingi duniani. Kwa hakika, upotoshaji wa taarifa pamoja na matukio makali ya hali ya hewa vimetajwa miongoni mwa hatari kubwa zaidi zinazoikabili jamii katika kipindi cha miaka miwili ijayo, kwa mujibu wa ripoti ya karibuni ya hatari za dunia kutoka World Economic Forum.[2] Hii ina maana kwamba waandishi wa habari wana jukumu muhimu katika kufichua madai ya uongo huku wakihakikisha hawachangii bila kujua kusambaa kwa taarifa hizo kupitia kuripoti bila kuthibitisha. Katika sehemu hii, tutaangalia jinsi unavyoweza kutekeleza jukumu hilo na kusaidia hadhira kujenga uimara dhidi ya upotoshaji na taarifa zisizo sahihi.

## 3.2 - Maana ya upotoshaji wa taarifa

Kabla hujakabiliana na tatizo, ni muhimu kuelewa unachokabiliana nacho. Hili ni muhimu kwa sababu kuelewa zaidi kuhusu aina ya taarifa potofu zinazotumwa kunaweza kukusaidia kufichua, kurekebisha na kuzuia zisienee. Haya ndiyo maneno muhimu:

- **Upotoshaji/Disinformation** ni pale mtu anaposambaza taarifa za uongo kwa makusudi. Lengo ni kuwadanganya watu na kuwafanya waamini kuwa wanachosema ni kweli. Pamoja na misinformation, hili ni neno linalotumika sana.
- **Upotoshaji/Misinformation** ni pale mtu anaposhiriki taarifa za uongo kimakosa (bila kukusudia). Msemaji halengi kuwadanganya watu kwa makusudi. Pamoja na disinformation, hili ni neno linalotumika sana.
- **Upotoshaji/Malinformation** hutokana na taarifa za kweli ambazo zinasambazwa kwa nia ya kusababisha madhara au aibu, kama vile anwani ya mtu.
- **Muktadha wa Uongo/False context** ni pale maudhui ya kweli yanaposambazwa tena nje ya muktadha wake wa awali.

Neno maarufu linalotumiwa sana na vyombo vya habari ni '**fake news**'. Epuka kutumia kifungu hiki kwa sababu mbili:
- Linatumiwa na wanasiasa wanaotaka kuepuka maswali magumu kutoka kwa waandishi wa habari
- Halielezi ipasavyo aina mbalimbali za upotoshaji wa taarifa ambazo waandishi wa habari hukabiliana nazo – kama zilivyoorodheshwa hapo juu

[1] *https://disinfo.africa/ignorance-and-faith-blur-tanzanias-climate-facts-3944ec758ecb*
[2] *https://reports.weforum.org/docs/WEF_Global_Risks_Report_2026.pdf*

## 3.3 - Kauli potofu kuhusu tabianchi

Katika somo hili tutaangalia:
- Ni wakati gani mtu atarajie kuongezeka kwa upotoshaji na taarifa potofu
- Ni kauli gani za uongo zinazoenea kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi nchini Tanzania
- Kwa nini watu wanaziamini

- **Wakati wa kutarajia kuongezeka kwa upotoshaji na taarifa potofu**

Upotoshaji na taarifa potofu kuhusu mabadiliko ya tabianchi husambaa kila wakati, lakini huwa mbaya zaidi katika nyakati fulani:
- Matukio makubwa ya hali mbaya ya hewa kama mafuriko au ukame. Hali huwa ya vurugu na kupata taarifa sahihi huwa kugumu.
- Mikutano ya kimataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi. Taarifa za uongo zinaweza kusambazwa na watu wenye maslahi binafsi kama baadhi ya kampuni kubwa, ambao huzipeleka kwenye majukwaa ya mitandao ya kijamii na vyombo vya habari vinavyowaunga mkono, pamoja na makundi ya kisiasa, kidini na ya kijamii.

- **Kauli potofu za kawaida**

Taarifa iliyoandikwa na African Digital Democracy Observatory (https://disinfo.africa/ignorance-and-faith-blur-tanzanias-climate-facts-3944ec758ecb) inafafanua matokeo ya uchunguzi uliobaini kauli tatu kuu zinazoathiri mijadala ya umma kwenye mitandao ya kijamii kuhusu mabadiliko ya tabianchi nchini Tanzania. Nazo ni:
- **Kauli za kukataa (Denial narrative)**. Kauli ya kukataa hudai kuwa mabadiliko ya tabianchi ni 'utapeli', sehemu ya 'ajenda ya Magharibi' au ni jambo la 'kiasili'.

**Mfano**: Mfano huu kutoka kwenye mtandao wa kijamii X unaodai kwamba volkano huzalisha hewa-ukaa ($CO_2$) zaidi kuliko binadamu ni upotoshaji unaorudiwa mara kwa mara, ambao katika kesi hii umeondolewa shaka na Africa Check kwa kutumia vyanzo vya kisayansi vinavyoaminika.




- **Masimulizi ya uhamishaji (Displacement narrative)**. Masimulizi ya uhamishaji yanalaumu matukio ya eneo husika (kwa mfano, ukataji miti) kuwa ndiyo chanzo pekee cha mafuriko bila kuangalia muktadha mpana wa mabadiliko ya tabianchi.
- **Masimulizi ya kidini/kiroho (Religious/spiritual narrative)**. Masimulizi ya kidini au kiroho yanaeleza majanga kama adhabu ya Mungu, yakipuuzia uhusiano wake na mabadiliko ya tabianchi au sababu nyingine za kimazingira.

- **Sababu za watu kuamini masimulizi ya uongo**

Kuna sababu kadhaa ikiwemo:
- Dai la uongo linakwenda sambamba na imani zao za kisiasa au kidini
- Wanapata taarifa sahihi kwa kiwango kidogo
- Kizuizi cha lugha*
- Taarifa inatoka kwa marafiki au familia hivyo kuhisi kuwa ni ya kuaminika zaidi

**Kuzungumza na watu kwa lugha wanayoielewa kama ilivyoelezwa katika Sehemu ya 1 kunamaanisha pia kuzungumza nao kwa lugha yao ya asili. Hata hivyo, misamiati ya sayansi ya tabianchi wakati mwingine haiwezi kutafsiriwa kwa uwazi au urahisi na inaweza kupotoshwa au kutoeleweka*.

Sababu ya mwisho – kwamba masimulizi ya uongo yanatoka kwa marafiki au familia hivyo kuonekana kuwa ya kuaminika zaidi – inaweza kuwa ngumu sana kwa waandishi wa habari kuipinga. Lakini inasaidia iwapo utatambua mbinu zinazotumiwa na wadanganyifu, jambo ambalo tutalichunguza hapa mbele.

### 3.4 - Jinsi ya kubaini upotoshaji wa habari

Zipo mbinu ambazo wale wanaosambaza upotoshaji wa habari hutumia na hurudia mara kwa mara ili kuwafanya watu waamini mambo ambayo si ya kweli. Wanasaikolojia katika Chuo Kikuu cha Cambridge nchini Uingereza wametengeneza kifupi cha maneno — **DEPICT** — ili kukusaidia kuvitambua.

- **D ni kwa ajili ya discrediting (kudhalilisha)**: Waandishi wa habari, vyombo vikuu vya habari na sayansi mara nyingi hulengwa kwa kupandikizwa shaka kuhusu uaminifu wao.
- **E ni kwa ajili ya emotion (hisia)**: Maudhui yanayochezea hisia za msingi kama hofu au hasira hupata uangalizi mkubwa zaidi.
- **P ni kwa ajili ya polarisation (mgawanyiko)**: Mgawanyiko wa kisiasa ni lengo kuu la kampeni za upotoshaji zinazolengwa, ambazo hutumia akaunti bandia kuusambaza.
- **I ni kwa ajili ya impersonation (kujifanya mtu mwingine)**: Kujifanya kuwa mtu mwingine mtandaoni, kwa mfano mwanasayansi wa tabianchi au chombo halali cha habari.
- **C ni kwa ajili ya conspiracy (njama)**: Nadharia za uongo zinazolenga mambo ambayo watu huyajali, kwa mfano, ufisadi wa kisiasa.
- **T ni kwa ajili ya trolling (ushambulizi wa mtandaoni)**: Waandishi wa habari mara nyingi hulengwa kwa maoni ya uchochezi ili kuchochea hasira za umma.

Kuna maelezo zaidi kuhusu kazi ya wanasaikolojia wa Chuo Kikuu cha Cambridge mwishoni mwa sehemu hii.

**Sylivester Domasa** ni meneja wa huduma za vyombo vya habari mtandaoni kwenye kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania (Tanzania Standard Newspapers) ambako anasema wanatumia mbinu hii: "*Tunalazimika kujiuliza, je, jambo hili linawezekana? Tunauliza swali hilo na tuna kanuni kwamba ukilishuku jambo, achana nalo.*"



### 3.5 - Pale waandishi wa habari wanapokuwa sehemu ya tatizo

- **Usawazishaji wa uongo (False balance)**

Kulingana na ripoti iliyoitwa *A study of climate journalism in East Africa in an Era of Misinformation ( Utafiti wa uandishi wa habari za tabia nchi Afrika Mashariki katika nyakati za upotoshaji)* theluthi mbili ya waandishi wa habari waliohojiwa wanasema "bado husawazisha habari zao kwa kutafuta vyanzo vinavyoeleza kuwa mabadiliko ya tabianchi yanatokea na yanasababishwa na binadamu, pamoja na wale wanaotia shaka hitimisho la kisayansi."[3]

Hii inajulikana kama usawazishaji wa uongo—wakati pande zote mbili za habari zinaonekana kana kwamba zina uzito sawa. Waandishi wa habari wanaotumia mtazamo huu wanakuwa sehemu ya tatizo kwa kuendeleza dhana potofu bila kuchunguza ni nani anayeieneza na nia yake ni nini. Mtazamo huu unaweza kupelekea hadhira kuamini kwamba wanasayansi wa tabianchi hawakubaliani kuhusu uhalisia wa mabadiliko ya tabianchi. Hiyo siyo kweli. Ukweli ni kwamba idadi kubwa sana ya wanasayansi wa tabianchi wanakubaliana kuwa mabadiliko ya tabianchi yanayosababishwa na binadamu ni ya kweli.

**Mikakati ya kuepuka usawazishaji wa uongo katika habari za mabadiliko ya tabianchi:**
- Kukumbusha hadhira kuhusu makubaliano ya kisayansi (kwa kunukuu, kwa mfano, ripoti za kisayansi)
- Kuchunguza uko wapi wale wenye shaka katika mizani ya kukanusha mabadiliko ya tabianchi—je, wanakana sayansi au wanauliza maswali kuhusu sera?
- Kuangalia kile ambacho sauti za wenye shaka zimekuwa zikisema kwenye mitandao ya kijamii
- Kutathmini kama ni sahihi na inafaa kumjumuisha mtu anayekana sayansi au kama unampa nafasi ya kueneza nadharia potofu

- **Kushiriki habari kwenye mitandao ya kijamii na programu za ujumbe**

Inaweza kuwa vigumu kutochapisha au kujibu habari zinazotrend kwenye mitandao ya kijamii au programu za ujumbe, hasa ukiwa chini ya shinikizo la kutengeneza habari. Lakini daima SIMAMA na FIKIRI KWANZA kwa sababu:
- Inaweza kudhuru uaminifu wa hadhira kwako na kwa chombo chako cha habari
- Inaweza kuwapa mamlaka sababu ya kuweka vizuizi kwenye uhuru wa vyombo vya habari

[3] https://earthjournalism.net/sites/default/files/2024-06/climate-misinformation-in-east-africa-september-2023_final_0.pdf


**Mfano:** Wataalamu wa ukaguzi wa ukweli, PesaCheck—wanaofanya kazi katika nchi 18 Afrika Mashariki, Afrika Magharibi na Sahel—walifichua kuwa video iliyokuwa ikisambazwa kwenye mitandao ya kijamii ikidai kuonyesha mafuriko makubwa Tanzania, kwa kweli ilirekodiwa katika mji mkuu wa Indonesia, Jakarta. Habari kamili: https://pesacheck.org/false-this-video-claiming-to-show-floods-in-tanzania-is-actually-from-indonesia/

### 3.6 - Kuimarisha uimara wa hadhira dhidi ya upotoshaji

Kukanusha taarifa—ambapo mwandishi wa habari hufichua uongo baada ya habari kuchapishwa—kunaweza kukatisha tamaa. Dai la uongo la awali linaweza kuwa limeshaonwa na maelfu au makumi ya maelfu ya watu kabla taarifa yako ya kukanusha haijachapishwa. Lakini fikiria kama ungeweza kufichua uongo kabla habari hizo hazijawafikia hadhira yako. Unaweza kufanya hivyo kupitia mbinu inayoitwa **prebunking**. Prebunking ni nini?

- Prebunking hufanya kazi kama chanjo ambapo waandishi wa habari huwafichua hadhira kwa mifano ya upotoshaji wa aina mbalimbali
- Prebunking huwasaidia watu kujenga kinga dhidi ya madai ya uongo kwa kuwasaidia kuyatambua kabla hawajakutana nayo
- Prebunking huwapa hadhira uwezo wa kufikiri kwa kina ili kupinga upotoshaji kwa kuwa waandishi wa habari tayari wamekanusha madai ya uongo mapema

Hali ikoje katika chumba cha habari?



Wakati wa janga la Covid-19, Africa Check ilichapisha maelezo mafupi yaliyotoa ukweli sahihi kuhusu mada ambazo mara nyingi hulengwa na taarifa potofu, kama vile chanjo.
Makala hii inaeleza jinsi ya kufanya prebunking kwa hotuba ya hali ya taifa bila hata kuiona kabla: https://africacheck.org/fact-checks/blog/how-pre-bunk-state-nation-address-and-almost-anything-else

### 3.7 - Kujenga ushirikiano

Kukanusha na kukagua ukweli bado ni ujuzi muhimu sana kwa mwandishi wa habari anayetaka kukabiliana na uenezaji wa upotoshaji wa makosa na wa makusudi. Hili linaweza kuwa kazi ngumu na ya kuchukua muda kwa mwandishi mmoja mwenye majukumu mengi, hivyo suluhisho moja ni kujenga ushirikiano na waandishi wengine na vyumba vya habari. Hapa kuna mifano:

- **Mikakati ya ukaguzi wa ukweli**

- Mashirika ya ukaguzi wa ukweli kama Africa Check, African Fact-Checking Alliance, Code for Africa, JamiiCheck, na PesaCheck hushirikiana na waandishi wa habari na vyombo vya habari pamoja na asasi za kiraia kupambana na uenezaji wa upotoshaji kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya tabianchi. (Viungo/link vipo mwishoni mwa sehemu hii).

- **Ushirikiano na wataalamu wa tabianchi**

- Aidha kupitia vyuo vikuu au mashirika kama ClimDev-Africa, World Federation of Science Journalists au Umoja wa Mataifa. (Viungo vipo mwishoni mwa sehemu hii).

- **Mafunzo na msaada**

- Kushirikiana na vyumba vingine vya habari kutoa rasilimali za mafunzo au kupata fursa kupitia mashirika kama Climate Action Network (CAN) Tanzania, Tanzania Media Foundation au Earth Journalism Network. (Viungo vipo mwishoni mwa programu).

### 3.8 - Zoezi

Jiweke katika hali hii kisha ujibu maswali. Majibu yapo mwishoni mwa sehemu hii.

*Unapokea ujumbe kutoka kwa rafiki kwenye kundi la WhatsApp anayekutumia chapisho la mitandaoni linalomuonyesha mwanasayansi wa tabianchi akisema mabadiliko ya tabianchi ni jambo la asili na halina uhusiano wowote na shughuli za binadamu. Anaonekana aliyasema wakati wa mahojiano kwa kuwa nembo ya chombo cha habari ipo kwenye nukuu hiyo. Ni kipindi cha kuelekea mkutano wa kilele wa Afrika kuhusu mabadiliko ya tabianchi, na rafiki yako anasema ni taarifa muhimu ambayo unapaswa kushiriki.*

**Swali la 1**. Kitu cha kwanza utakachofanya ni nini?

A. Kutuma chapisho hilo kwenye mitandao ya kijamii na WhatsApp
B. Kuandika habari kuhusu nukuu hiyo kwa ajili ya chombo chako cha habari
C. Kuanza kuchunguza kama nukuu hiyo ni ya kweli

**Swali la 2**. Unaweza kuwasiliana na nani ili kuthibitisha kama nukuu hiyo ni ya kweli? Chagua wawili kutoka kwenye orodha hapa chini.

A. Rafiki yako
B. Mhariri wako
C. Mwanasayansi aliyenukuliwa
D. Chombo cha habari ambacho nembo yake imetumika
E. Hakuna, kwa sababu unaamini uamuzi wako mwenyewe

**Swali la 3**. Unagundua kuwa chapisho la mitandaoni ni la uongo. Unaweza kufanya nini ili kuzuia taarifa hiyo potofu kuendelea kusambaa?

A. Hakuna, tayari limeshasambaa
B. Kuandika habari na kuishiriki kwenye majukwaa ambako chapisho la uongo linasambazwa ili kueleza kwa nini si la kweli na namna unavyoweza kuthibitisha
C. Kuwasiliana na jukwaa la mitandao ya kijamii ambako lilichapisha awali

**Swali la 4**. Mhariri wako anauliza kama hili ni chapisho la mara moja tu au kuna uwezekano wa kuwepo upotoshaji zaidi unaozunguka kabla na wakati wa mkutano wa kilele kuhusu mabadiliko ya tabianchi. Ungejibu nini?

A. Kuna uwezekano mkubwa kutakuwa na mengine ukizingatia kilichotokea katika mikutano ya awali
B. Hakuna njia ya kujua
C. Ni tukio la mara moja

**Swali la 5**. Mhariri wako kisha anauliza ni mbinu gani bora zaidi ya kukabiliana na uenezaji wa upotoshaji kabla na wakati wa mkutano wa kilele? Unashauri nini?

A. Kuukanusha upotoshaji unapoonekana
B. Kuupuuzia
C. Kufanya *prebunking* kabla mkutano haujaanza kwa kuiambia hadhira masimulizi potofu makuu wanayoweza kusikia

## 3.9 - Mambo ya msingi ya kukumbuka

Umefika mwisho wa sehemu hii. Hapa kuna ukumbusho wa mambo matatu muhimu uliyojifunza:

**Jambo muhimu la kuondoka nalo la 1**: Kuelewa mbinu za upotoshaji kutakusaidia kukabiliana nazo kwa ufanisi zaidi
**Jambo muhimu la kuondoka nalo la 2**: Kuepuka usawazishaji wa uongo na kuwakumbusha watu kuhusu makubaliano ya kisayansi juu ya mabadiliko ya tabianchi
**Jambo muhimu la kuondoka nalo la 3**: Kuwawezesha watu kwa kufichua na kufanya prebunking kwa madai ya uongo wanayoweza kusikia

## Vyanzo vya Taarifa


### Za Jumla
- DigihubAfrica: https://www.digihubafrica.org/
- Thomson Foundation | Rethinking Disinformation: psychology, prebunking and other tactics to halt the spread: https://www.journalismnow.org/course/rethinking-disinformation-psychology-prebunking-and-other-tactics-to-halt-the-spread

### 3.4 - Jinsi ya kutambua taarifa potofu
- University of Cambridge Social Decision-Making Lab: https://www.sdmlab.psychol.cam.ac.uk/

### 3.6 - Kuimarisha uimara wa hadhira dhidi ya upotoshaji
- A practical guide to prebunking misinformation: https://prebunking.withgoogle.com/docs/A_Practical_Guide_to_Prebunking_Misinformation.pdf

### 3.7 - Kujenga ushirikiano
- Africa Check: https://africacheck.org/
- African Climate Change Experts: https://uneca.org/african-climate-policy-centre/african-climate-change-experts
- Africa Fact-Checking Alliance: https://factcheck.africa/about-afca-658670a36eb5
- Climate Action Network Tanzania: https://cantz.or.tz/
- Climate-Uni.com: https://www.climate-uni.com/tanzania-team
- Code for Africa: https://codeforafrica.org/
- Earth Journalism Network: https://earthjournalism.net/
- PesaCheck: https://pesacheck.org/
- World Federation of Science Journalists: https://wfsj.org/

### Majibu ya Zoezi la 3.8

**Swali la 1**. Jibu sahihi ni c. Unaweza kushinikizwa na rafiki au mtu mwingine kuandika taarifa, lakini unapaswa kuthibitisha ukweli kwanza. Kamwe usishiriki chochote bila kujua kuwa ni sahihi.

**Swali la 2**. Majibu sahihi ni c na d. Mwanasayansi anaweza kuthibitisha kama kweli aliyasema maneno hayo, na chombo cha habari kinaweza kuthibitisha kama yalitamkwa wakati wa mahojiano au kama nembo inayotumiwa ni ya kughushi.

**Swali la 3**. Jibu sahihi ni b. Huu ni mtazamo wa kimkakati unaoiwezesha hadhira yako kuona mbinu zinazotumiwa kuunda upotoshaji.

**Swali la 4**. Jibu sahihi ni a. Upotoshaji wa makosa na wa makusudi huongezeka wakati wa mikutano ya kimataifa ya mabadiliko ya tabianchi.

**Swali la 5**. Jibu sahihi ni c. Kukanusha (debunking) bado ni muhimu, lakini prebunking inaweza kusaidia kujenga kinga na uimara wa hadhira dhidi ya upotoshaji kabla hata haujawafikia.

# Sehemu ya 4 - Kuripoti habari za mabadiliko ya tabia nchi kwa usalama

## 4.1 - Kutathmini hatari

Kujaribu kuwawajibisha wenye mamlaka kunaweza kuja na gharama kwa waandishi wa habari. Baadhi ya habari zinaweza kuwa hatari kuhabarisha umma kuliko nyingine na hii haswa hujitokeza katika uandishi wa habari za mazingira, ambao unahusisha habari za mabadiliko ya tabia nchi. Kama tulivyojifunza hapo kabla katika kitini hiki, vipo vichocheo vya kisiasa na kiuchumi kama vile rushwa kwa habari zinazohusiana na majanga yanayohusiana na mabadiliko ya tabia nchi na upatikanaji wa rasilimali kama vile chakula na maji safi. Waandishi wanaweza kukabiliwa na vitisho vya usalama wao au kuhujumiwa taarifa walizoandaa au kurekodi. Zipo hatari za nyongeza wakati wa kuandaa taarifa za matukio mabaya ya hali ya hewa kama vile mafuriko na dhoruba.

Katika sehemu hii utasaidiwa kutathmini hatari na kupewa dondoo za jinsi ya kubakia salama. Pia utapatiwa ushauri kuhusu haki zako za kisheria.

## 4.2 - Ni kwa nini tathmini ya hatari ni muhimu?

Sababu zinazofanya baadhi ya waandishi wa habari na wahariri kutochukulia suala la tathmini ya hatari kwa uzito unaostahili zinaweza kuwa ni pamoja na:

- Kutokuelewa nini maana ya tathmini ya hatari
- Kuamini kuwa dhamira njema au bahati vinatosha
- Ina gharama kubwa
- Inachukua muda mrefu

Ukweli ni kwamba zipo hatari katika kila habari unayoweza kuiandaa, hususani wakati mabadiliko ya tabia nchi yanapohusika na uandaaji wa habari ya matukio mabaya ya hali ya hewa au maandamano katika mkutano wa kilele wa mabadiliko ya tabia nchi. Kubainisha hatari unazoweza kukutana nazo kabla ya kwenda kuandaa habari kunaweza kukusaidia kuwa salama na kukabiliana na mazingira kadri yanavyobadilika.

**Hassan Mhelela** ni mhariri mkuu wa Televisheni ya Azam iliyopo jijini Dar Es Salaam. Ameshafundisha waandishi na wahariri nchini kote Tanzania katika masuala ya usalama wa kimwili na kidijitali na umuhimu wa kutathmini hatari. Amekuwa akiwahamasisha kuzingatia angalau matabaka matatu ya kutathmini hatari.



"***Tabaka la kwanza*** *linahusu usalama wa jumla. Unaweza kuwa usalama wa barabarani: magari wanayotumia kufukuzia habari, kama madereva wana bima, magari yako katika hali nzuri, wanaweza kufikiri kuhusu kuandaa ramani ya njia watakazopitia kabla ya kuondoka.* ***Tabaka la pili*** *la kutathmini hatari linaweza kuhusu sababu za nje. Kwa mfano, maeneo wanayotembelea, je ni salama? Je tutatambua matukio yaliyopita ambayo yamerikodiwa au kutolewa taarifa?* ***Tabaka la tatu*** *ni kama usalama wao unaweza kuhusisha vyombo vya ulinzi na usalama …Uchaguzi mkuu mara zote ni wakati muhimu. Tunatambua kuwa mchezo wa mpira wa miguu unaweza kuathiri hali ya utulivu na usalama wa umma hivyo tunawataka waandishi wa habari za michezo kujiandaa mapema, hata kufikiri kuhusu wapi pa kukaa na kuwa na mpango wa kukimbia kama ikitokea mkusanyiko wa watu unageuka kuwa tatizo."*
(Hassan Mhelela)

## 4.3 - Je hatari inaonekanaje?

Kuwa na uwezo wa kubainisha hatari unazoweza kukutana nazo ni eneo la kuanzia. Hebu zingatia mazingira haya.

- **Mafuriko**

Kuna taarifa za mafuriko makubwa baada ya mvua kubwa. Unakwenda peke yako sehemu ambazo zimeathirika zaidi na bila kumfahamisha mtu. Chukua muda mfupi kufikiri kuhusu ni hatari gani unaweza kukabiliwa nazo halafu angalia mapendekezo ya chini ya picha hii hapa chini.



- Unaweza kukwama kwenye maji ya mafuriko
- Simu yako na vifaa vya kurekodia vinaweza kulowa maji na kuharibika
- Unaweza kukwama bila kuwa na chakula au maji
- Unamweka mtu mwingine katika hatari kama unapanga kukutana nae
- Hujamwambia mtu yoyote wapi umeenda

- **Maandamano**

Wanaharakati wa mabadiliko ya tabia nchi wanaandamana katika eneo la ndani ndani mbali na makazi ambako wakataji magogo haramu wanaendesha shughuli zao. Polisi pia wapo hapo. Unakodisha gari kwenda kuandaa habari ya tukio hilo ukiwa peke yako.

Chukua muda mfupi kutafakari ni hatari gani unaweza kukabiliwa nazo halafu angalia mapendekezo chini ya picha.



- Unaweza kupata ajali wakati unaendesha gari na kugundua huna bima ya kukusaidia katika hali inayoonekana kuwa ya hatari.
- Uko katika maeneo ya ndani ndani mbali na makazi ya watu ambako huwezi kupata chakula wala maji ya kunywa
- Unaweza kukamatwa na polisi ambao wanaweza kukunyang'anya vifaa vyako vya uandishi wa habari ulivyokuwa unatumia kuchukulia picha na kurekodi maandamano
- Unaweza kujeruhiwa kutokana na kuwa sehemu isiyofaa wakati wa maandamano
- Unaweza kujikuta unakuwa mlengwa wa baadaye wa makundi ya magenge ya wahalifu

Orodha ya hatari zinazoweza kujitokeza haitakiwi kukutisha. Inaweza isijitokeze hata hatari moja. Unaweza kuwa mwenye bahati. Lakini je unataka kutegemea bahati pekee ili kuwa salama? Ushauri huu unatumika iwapo wewe ni mwandishi wa kujitegemea, mwandishi wa mkataba mfupi au mwandishi mwajiriwa au mhariri mwenye dhamana ya usalama wa timu yako. Pia tambua kuwa hatari zinaweza kubadilika wakati unaenda kufanyia kazi habari kwani mazingira hubadilika. Unapaswa kuwa tayari kutathmini upya hatari zinazoweza kukukabili. Punde tu unapokuwa umeshabainisha hatari hizo, hatua inayofuata ni kufikiri nini cha kufanya ili wewe, vifaa, waandishi wenzako na watu utakaowahoji muweze kuwa salama.

### 4.4 - Tathmini ya hatari ikoje?

Kimsingi, tathmini ya hatari ni maswali ambayo unapaswa kujiuliza kabla ya kwenda kuandaa habari. Kanuni za msingi ni:

- **Panga** – je habari ni ipi na utaiandaaje?
- **Jiandae** – je una vifaa muhimu ambavyo utahitaji kuwa salama?
- **Tabiri** – je ni nini kinaweza kuharibika na nini unaweza kufanya kushughulikia tatizo?

Fomu ya Tathmini ya Hatari iko katika Kiambatisho. Itumie kama msingi wa kutengeneza fomu yako. Wahariri wanaweza kutumia mbadala wake kutengeneza fomu moja kwa ajili ya kutumika katika chombo cha habari. Upo mwongozo kwa kifupi juu ya fomu ukielezea jinsi ya kuijaza. Siyo lazima tathmini ya hatari ikugharimu pesa au muda mwingi kwani unatathmini hatari unazoweza kukabiliana nazo na jinsi gani ya kuzitatua. Hapo chini ni baadhi ya masuala unayoweza kuzingatia japo siyo yote yatakuwa yanafaa kwa kila habari.

**Wapi ninakwenda na nitafikaje huko?**

- Je barabara ni salama? Angalia ushauri wa kusafiri kabla ya kuondoka. Kwa mfano, baadhi ya barabara zinawezekana kutopitika katika mafuriko
- Je gari linafaa kuwa barabarani?
- Je gari lina bima ya changamoto zote zinazoweza kujitokeza? Je nahitaji msaidizi mwenyeji wa eneo hilo kwa ajili ya ushauri?

**Ni vifaa gani nitahitaji?**

- Mara zote beba chakula, maji, nguo za akiba na vifaa vingine kama kamba ya kuvutia gari na vifaa vya kuchimbia ili kujiepusha na shida
- Ni aina gani ya vitambulisho nitahitaji? Kumbuka Kadi ya Uandishi wa habari/Pasipoti
- Siku zote beba kitini cha huduma ya kwanza

**Utavaa nini?**

- Tafakari kuhusu nguo za kufanyia kazi na viatu. Unaweza kuhitaji kutembea umbali mrefu
- Je utahitaji nguo za kukulinda kama ikitokea maandamano au kushambuliwa?

**Je una mpango gani wa usalama wa kidijitali?**

- Ni hatua gani utachukua kulinda maudhui uliyochukua kwa kamera au simu ya kiganjani? Somo zaidi lipo baadaye katika sehemu hii
- Je nahitaji zaidi ya simu janja moja? Moja kwa ajili ya maudhui, nyingine kwa ajili ya kupiga simu?
- Ni vifaa kiasi gani naweza kubeba na kuweza kuendelea kutembea vizuri?
- Ni jinsi gani nitatuma taarifa zangu kwenye chumba cha habari au kwa mfanyakazi mwenzangu ninayemwamini? Somo zaidi litakuja baadaye katika sehemu hii

**Nawezaje kujiokoa kama nikikutwa na shida?**

- Mara zote kuwa na mpango wa kujiokoa/jinsi ya kutoka. Je maji ya mafuriko yanaendelea kuongezeka, je barabara uliyokuja nayo inaweza kufungwa? Je ni eneo gani la kutokea kutoka kwenye maandamano? Angalia Ramani za Google, uliza ushauri kutoka kwa wenyeji kabla ya kutoka
- Mkakati wa kutoka kama niko kwenye jengo ni upi? Katika hoteli tafuta eneo la kutokea kama kuna janga la moto, usipende kukaa katika vyumba vya hoteli juu ya mapokezi ambavyo vinaweza kushambuliwa kiurahisi kwa mabomu
- Kama kuna dharula, kubaliana na chumba chako cha habari kuwapa taarifa kwa ujumbe wa alama za kieletroni (coded) kuwa uko kwenye matatizo

**Watu watajuaje niko wapi?**

- Mara zote mtaarifu mhariri wako au mwandishi mwenzako unayemwamini juu ya unakok-wenda
- Endeleza mawasiliano. Zingatia kuandaa kabla muda wa kuhabarisha chumba chako cha habari juu ya yanayoendelea
- Kama utapoteza simu yako, muda wote beba namba za dharula katika karatasi au nyar-aka ngumu

Kamati ya Kulinda Waandishi wa Habari (The Committee to Protect Journalists (CPJ) pia wana fomu ya kutathmini hatari ambayo ipo mwisho wa somo hili. https://cpj.org/wp-content/uploads/2020/08/CPJ-Emergencies_Risk-Assessment-Template-2.pdf.

## 4.5 - Ulinzi na usalama wa kidijitali

Kuwa muwazi sana kuhusu usalama wa kidijitali na kuchukua hatua za kutosha kunaweza kupelekea wewe, vyanzo vyako na timu nzima kufikiwa kirahisi na mtu yoyote anayehitaji taarifa zako. Hivyo sambamba na usalama wa kimwili, ulinzi na usalama wa kidijitali ni sehemu muhimu katika tathmini yoyote ya hatari.

- **Tathmini ya ulinzi na usalama wa kidijitali**

Tafakari kuhusu:
- Nani anaweza kufikia vifaa vyangu
- Nawezaje kuweka salama taarifa zangu zilizorekodiwa katika vifaa vyangu
- Nawezaje kulinda taarifa zozote zile zilizorekodiwa katika vifaa vyangu
- Nawezaje kutuma taarifa zangu kwenda kwenye chumba cha habari



**Hassan Mhelela** ambaye ni mhariri mkuu wa Televisheni ya Azam TV jijini Dar Es Salaam anatoa mafunzo ya usalama wa kidijitali kwa waandishi wa habari. Hizi ndizo mada zake kuu:

- Usitumie teknolojia ya mwili (alama za vidole au uso) kufungulia kifaa chako. Ni rahisi mtu kukushinikiza kukifungua
- Nywila ndefu yenye herufi na namba ina usalama zaidi
- Inawezekana kuandaa baadhi ya vifaa kufuta maudhui yote kama nywila isiyo sahihi ikiingizwa mara kadhaa
- Tumia programu isiyoruhusu ujumbe kuonekana na watu wa kati (end-to-end encrypted) kama vile Signal kutuma ujumbe wako
- Tambua kuwa matumizi ya VPNs (virtual private networks) bila ruhusa ya mamlaka za mawasiliano ni kinyume cha sheria nchini Tanzania
- Njia nyingine salama za kutuma taarifa zako nyeti ni kwa: OnionShare – programu ya bure ambayo inawezesha kutuma mafaili au kuongea na wengine bila kujulikana. Inatumia mtandao wa Tor – programu ya bure ya kuvinjari mtandaoni

Hassan anaonya kuwa waandishi wa habari mara nyingi wanagusa haraka viunganishi vya mtandaoni (links) walivyopelekewa bila kujua kama wavuti zao ni salama. Anaonya:
- Kugusa mara moja tu wavuti ambayo siyo salama kunaweza kuangamiza chumba kizima cha habari
- Mara zote angalia kiunganishi kabla hujafungua
- Usidhani kuwa kwa kuwa kiunganishi kimetumwa na chanzo chako cha taarifa ni salama kukifungua

Vipo viunganishi vya kuhakiki wavuti katika sehemu ya mwisho mwa somo hili.

**Usitangaze mahali ulipo:** Kama unafanyia kazi habari nyeti, usiitume kwenye mitandao ya kijamii hadi unapokuwa umeondoka eneo hilo. Unaweza kufuatiliwa na hivyo kukuweka kwenye hatari na vyanzo vyako vya taarifa.

- **Kushughulika na udhalilishaji wa mtandaoni**

Mashambulizi ya mtandaoni dhidi ya waandishi nchini Tanzania, hususani wanawake yanaripotiwa kuongezeka. Mashambulizi haya yanaweza kukutisha, kuleta hofu na mara nyingine kukuzidi nguvu. Wakati wadhalilishaji wengi mtandaoni wanafanya kazi wakiwa peke yao, wanaweza kuwa sehemu ya kikundi kinachofanya kazi na wafanyabiashara wakubwa, magenge ya kihalifu au serikali. Kila aina ya tathmini ya hatari inapaswa kuzingatia maswali juu ya uwepo wa waandishi mtandaoni.

- Weka kumbukumbu ya udhalilishaji na kupiga picha
- Usiwajibu wadhalilishaji kwani unaweza kuyapa nguvu mambo yao waliyochapisha na hilo ndilo wanalolitafuta
- Waombe waandishi wenzako kufuatilia mitandao ya kijamii kama udhalilishaji unajitokeza kwa wingi kuweza kuufuatilia kila siku
- Wafungie watu wanaodhalilisha mtandaoni

## 4.6 - Ushauri wa kisheria

Uandishi wa mabadiliko ya tabia nchi Tanzania mara nyingi unaambatana na masuala nyeti kama vile migogoro ya ardhi, sekta ya madini, migogoro ya uhifadhi na maandamano ya wananchi. Mazingira kama haya yanawaweka waandishi wa habari katika hatari za kisheria, ikiwa ni pamoja na kukamatwa, kunyang'anywa vifaa, au kulazimishwa kutoa taarifa za vyanzo vyao vya habari. Waandishi wengi hawajafundishwa sheria na mashirika mengi ya habari hayawezi kulipia gharama za kisheria – lakini inawezekana vyumba vya habari kuchangia gharama ili kuwa na mtu wanayeweza kumwita kwa ajili ya ushauri au msaada unapohitajika. Pia vipo viunganishi vya mashirika yanayotoa ushauri wa kisheria bure kwa waandishi wa habari mwishoni mwa somo hili. Kuwa na mwongozo wa kisheria kunaweza kuimarisha kuaminiwa kwa taaluma yako na ulinzi wa kisheria.

Hebu fikiria kuwa wewe ni mwandishi wa habari unayeandaa habari ya maandamano ya mabadiliko ya tabia nchi, nini kitatokea kama utakamatwa na polisi au polisi watajaribu kuchukua simu yako au kamera? Utafanya nini na utaomba msaada kutoka wapi?

- **Haki na wajibu wako**

Sheria zinazidi kutumiwa dhidi ya waandishi wa habari wa mazingira duniani kote ili kuwadhoofisha, kuwazuia au kuwatishia. Hii ndiyo sababu tathmini ya hatari inayohusu usalama wa kimwili na kidijitali ni muhimu. Waandishi wa Habari nchiini Tanzania wana haki za kisheria na wajibu pia kama inavyoelezewa hapo chini.

**<u>Uhuru wa kujieleza</u>**

Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) inamhakikishia kila mtu uhuru wa maoni na kujieleza, ikiwa ni pamoja na kutafuta, kupata na kusambaza taarifa. Ulinzi huu unahusu pia waandishi wanaoandika habari za maslahi ya umma, ikiwa ni pamoja na mazingira na mabadiliko ya tabia nchi. Hata hivyo, haki za kikatiba zina ukomo, na zinaweza kukinzana na maslahi ya usalama wa taifa, utulivu wa umma, maadili, au usalama wa ujumla. Unapojijitetea kwa kutumia haki za kikatiba unapaswa kufanya hivyo kwa weledi na bila kutumia nguvu.

**Ushauri**: Iwapo utasimamishwa kuendelea kuandika habari: kuwa mtulivu, wasilisha utambulisho halali, uliza ni kwa sheria gani kizuizi hicho kinafanyika, weka kumbukumbu za mjadala kama ni salama, na mhabarishe mhariri wako au mshauri wa kisheria.

**Mapendekezo ya maelezo toka uwandani (field):** "*Mimi ni mwandishi wa habari ninayetumia haki zangu za kikatiba kukusanya na kusambaza taarifa chini ya Ibara ya 18 ya Katiba. Je unaweza kunifafanulia misingi ya kisheria ya kuzuia kazi yangu?*"

**Kukusanya taarifa**

Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari inatoa muongozo wa kisheria juu ya utambulisho, leseni, maadili na mienendo ya kiweledi kwa waandishi wa habari nchini Tanzania. Waandishi waliopatiwa vitambulisho kufanya kazi za uandishi wanaofanya kazi chini ya vyombo vya habari wanatambuliwa kisheria kukusanya taarifa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali.

**Wajibu wako wakati wa kukusanya taarifa:**
- Kitambulisho lazima kiwe kinafanya kazi wakati huo
- Kuandika habari kutoka maeneo tengefu, misitu, madini, maeneo ya hifadhi au maeneo mengine yanayodhibitiwa kisheria kunaweza kuhitaji kibali kingine mbali na vibali vya uandishi wa habari
- Sheria inakataza kuchapisha taarifa za uchochezi, za uongo, na zinazotishia ulinzi na usalama wa taifa, au maudhui yanayochochea ghasia

**Wajibu wako unapochapisha habari zenye matokeo makubwa kimazingira:**
- Hakikisha unakuwa na ushahidi wa kimaandishi wakati wote
- Tumia kwa usahihi madai yanayotoka kwenye vyanzo vya taarifa
- Tumia lugha inayobadili maana ya sentensi kama vile "alidai" wakati uchunguzi unapokuwa unaendelea
- Toa nafasi na weka kumbukumbu ya haki ya kujibu
- Chunguza na thibitisha nyaraka za kisheria kwa habari ya kiuchunguzi yenye hatari kubwa

**Ushauri:** Waandishi wa habari wanapaswa kufanya kazi huku wakiwa na ufahamu wa sheria, taratibu na kanuni na utamaduni wa kuweka kumbukumbu. Vikwazo vya kiutawala (kama vile faini, kusimamishwa au kufutiwa usajali) vinaweza kujitokeza kabla ya utaratibu wa kimahakama.

**Vyanzo vya habari vya siri**

(Marekebisho) ya Kanuni za Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari yanawataka waandishi wa habari kufuata maadili ya kulinda vyanzo vya taarifa vya siri. Sheria za Tanzania zinatambua usiri katika uandishi wa habari. Hata hivyo, ulinzi huu una ukomo:

- Utoaji wa taarifa za siri za chanzo cha habari unaweza kushinikizwa na amri ya mahakama
- Utoaji wa taarifa unaweza kuonekana pia ni wa muhimu kama jambo linahusiana na usalama au uchunguzi wa kosa kubwa la jinai
- Sheria haitoi maslahi yoyote ya kidijitali kwa waandishi wa habari

**Ufafanuzi wa kivitendo**
Vyanzo vya taarifa vinaweza kutarajia usiri kama:

- Mahakama itatoa amri ya kushinikiza kutolewa kwa taarifa hizo
- Suala linahusu shughuli za kihalifu au usalama wa nchi
- Jaji anafahamisha kuwa kutolewa kwa taarifa hizo ni muhimu kwa ajili ya kusimamia haki
- Haihusiki katika hali ambapo chanzo cha taarifa kimehusika moja kwa moja katika shughuli za kihalifu. Usalama wa kina au uchunguzi vinaweza kutumika

**Ushauri:**

- Usiahidi kwa chanzo cha taarifa kuwa kutakuwa na usiri kamili bila kuelezea ukomo wa kisheria
- Elezea vyanzo vya taarifa mazingira ambapo taarifa za siri zinaweza kutolewa
- Hifadhi taarifa zinazobainisha vyanzo vyako katika sehemu tofauti na ilikofichwa ile ya kieletroniki
- Tumia majukwaa ya mawasiliano yenye usalama
- Kama ukishinikizwa bila utaratibu, omba kupitishwa kwenye mfumo rasmi wa kisheria

**Mapendekezo ya maelezo toka uwandani (field) kama mwandishi ameshinikizwa kutoa taarifa za chanzo cha taarifa:** "*Nina wajibu wa kitaaluma na kisheria kulinda vyanzo vya taarifa. Ninaomba madai yoyote ya kutoa taarifa za chanzo kutolewa kwa mfumo maalum wa kimahakama.*"

**<u>Nini kitatokea kama ukikamatwa?</u>**

Kwa mujibu wa Katiba na utaratibu wa sheria za jinai, mwandishi wa habari ana haki ya kuelezwa sababu ya kukamatwa, kupelekwa mahakamani katika muda unaofaa (katika kipindi cha masaa 24), kupata mwanasheria, kubakia kimya labda kwa taarifa za utambulisho, na kuwa huru dhidi ya utesaji au matendo ya kutweza.

**Ushauri:** Waandishi wa habari wasitumie nguvu kujilinda, kufuta picha au taarifa, kusaini hati bila kuhakiki kisheria, au kutoa taarifa za vyanzo vya taarifa vya siri.

**Mapendekezo ya maelezo toka uwandani (field):** "*Mimi ni mwandishi wa habari ninayefanya kazi zangu za uandishi. Tafadhali nielekeze msingi wa kisheria wa kukamatwa. Naomba kupata mwanasheria.*"

**<u>Ni nini hutokea wakati umepokonywa vifaa vyako?</u>**

Kupokonywa vifaa kunaweza kujitokeza chini ya uchunguzi wa jinai, waranti ya mahakama, sheria za usalama wa taifa au uchunguzi wa makosa ya mtandaoni.
Kanuni za jumla ni:

- Waranti inahitajika kufanya upekuzi wa chumba cha habari au makazi binafsi
- Upekuzi unaohusiana na kukamatwa au vifaa vinavyotaka kutumika kama ushahidi wa kosa la jinai linaloendelea unaweza kuhitaji waranti
- Wanaohusika na upokonyaji wa vifaa lazima wawekwe kwenye kumbukumbu

**Ushauri:**

- Usipambane kimwili
- Omba nyaraka za maandishi za kupekuliwa kwako
- Rekodi majina ya maofisa na namba za beji zao kama ni salama
- Mtaarifu mhariri wako na omba msaada wa kisheria haraka sana

**Mapendekezo ya maelezo toka uwandani (field):** "*Je kuna waranti inayoruhusu upekuaji au upokonyaji wa vifaa?*"

**<u>Je unatakiwa kufungua simu yako bila waranti?</u>**

Sheria za Tanzania, hazijajumuisha kabisa msaada wa kisheria wa kidijitali kwa mwandishi wa habari.

**Ushauri**:

- Usifungue vifaa vyako kwa hiari bila kutakiwa hivyo na mamlaka ya kisheria
- Omba kwa upole kuwa kila upekuzi ufuate mchakato rasmi wa kisheria
- Tumia ywila yenye nguvu badala ya alama za mwili (mfano vidole)
- Hakikisha kuwa taarifa zako kwenye kifaa zina ulinzi kamili wa kielektroniki

**Mapendekezo ya maelezo toka uwandani (field):** "*Naomba kwamba kila upekuzi wa kifaa changu ufuate utaratibu rasmi wa kisheria.*"

**<u>Sheria kwa ufupi</u>**

Mfumo wa sheria za Tanzania unatoa ulinzi wa kikatiba na pia kuwa na udhibiti wa kisheria kwa utendaji wa vyombo vya habari.

Katika uandishi wa habari za Mazingira, hatari haitokani na suala lenyewe, bali hutokana na kugongana na utawala, rasilimali, uchumi, maandamano na masuala ya usalama. Waandishi wa Habari ni lazima:

- Wawe na uelewa wa kisheria
- Wawe na nidhamu ya kiutaratibu
- Walinde utendaji wa taarifa zao
- Wawe na maadili ya kitaaluma

Baraza la Habari Tanzania limetengeneza maadili ambayo yanahusu mwenendo wa waandishi wenye taaluma ambao unapaswa kuzingatiwa. Kipo kiunganishi cha maadili hayo mwisho wa somo hili. Vilevile, ipo orodha ya rejea na masomo ya kisheria katika Kiambatisho.

### 4.7 - Zoezi – Maporomoko ya udongo

Fikiria kwamba unaandaa habari katika mazingira halafu jibu maswali.

*Kumekuwa na maporomoko makubwa ya udongo katika mji kilomita 30 kutoka ulipo. Makazi ya watu yameharibiwa na kuna taarifa za awali kuwa kuna watu wameuawa. Maporomoko hayo yamekuja baada ya dhoruba kali ambayo imeshasababisha uharibifu mkubwa. Unataka kuandika habari kwa ajili ya chombo chako cha habari. Zingatia haya maswali halafu utapata majibu hapo chini mwisho wa mafunzo.*

**Swali 1**. Ni jambo gani utafanya kwanza?

A. Unashuka kutoka kwenye gari lako na kwenda moja kwa moja kwenye eneo la tukio
B. Ongea na mhariri wako kuhusu njia ya kiusalama zaidi ya kuendelea na kazi yako

**Swali 2**. Jaza fomu ya tathmini ya hatari iwapo umeongea na mhariri wako na kukubalika kuwa unaweza kwenda kwenye mazingira ya tukio ili kuonyesha utazingatia hatari zipi? **Dondoo**: kuna jibu zaidi ya moja.

A. Je gari langu linafaa kwa safari barabarani?
B. Je barabara zinapitika?
C. Ni nguo gani utahitaji kubeba?
D. Ni vifaa gani utahitaji?
E. Nitawezaje kutunza vifaa vyangu vya kazi na kutuma taarifa zangu kwa usalama?
F. Nitawasiliana na nani kwa msaada?

HABARI MPYA

*Unafika katika mji ambapo watu wanakuambia kuwa dampo la taka katika eneo la karibu limeathirika na maporomoko ya udongo. Wanasema hali hiyo imesababisha taka sumu kuvuja na kuingia kwenye mfumo wa maji safi na watu wameshaanza kuugua. Wakazi wa eneo hilo walifanya kampeni hapo kabla kupinga dampo hilo wakidai limewekwa karibu mno na makazi yao. Wanaamini maofisa wa serikali za mitaa wala rushwa waliruhusu dampo hilo.*

**Swali 3**. Habari hii ni muhimu sana kuendeleza habari yako na taarifa mpya. Ni kitu gani utafanya kwanza?

A. Wasiliana na mhariri wako na kumweleza unawezaje kuthibitisha habari yako na kama utahitaji msaada na usalama zaidi wa kidijitali
B. Nenda katika ofisi za utawala za eneo hilo na kuwakabili
C. Hutafanya kitu, umekwenda kuandika habari za maporomoko ya udongo tu

**Swali 4**. Kuna taarifa kuwa mfumo wa maji safi katika eneo hilo unaweza kuwa umeharibiwa na sumu, ni hatari gani nyingine unakabiliwa nazo? Jibu majibu mengi unayodhani ni sahihi.

A. Hakuna
B. Unaweza kupata magonjwa kwa kunywa maji hayo
C. Nguo zako zinaweza kuchafuliwa na sumu kwenye maji hayo

**Swali 5**. Mabadiliko ya tabia nchi yanamaanisha matukio mabaya ya hali ya hewa (na matokeo yake kama vile maporomoko ya udongo) yanayozidi kujitokeza mara kwa mara. Unapaswa kuboresha zaidi tathmini yako ya hatari kuhakikisha unazingatia mazingira yanayobadilika na hatari unazoweza kukabiliwa nazo. Nani anaweza kukusaidia kwa jambo hilo?

A. Hakuna wa kukusaidia kwani una ufahamu wa kutosha
B. Huduma za dharula
C. Mhariri wako
D. Waandishi wenzako ambao wana uzoefu wa kuandika habari za majanga kama hayo
E. Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs)

### 4.8 - Mambo muhimu ya kuondoka nayo

Umefika mwisho wa somo hili. Jikumbushe mambo makuu matatu muhimu uliyojifunza.

**Jambo la 1**: Bainisha hatari unazoweza kukutana nazo KABLA ya kutoka au kumpeleka mtu kwenda kuandaa habari
**Jambo la 2**: Usalama ni jambo muhimu zaidi kwako, waandishi wenzako na vyanzo vyako vya taarifa. Usilifanye ni jambo la kuzingatia pale tu unapopata nafasi
**Jambo la 3**: Tafakari kuhusu sheria na tambua haki na wajibu wako chini ya sheria

## Vyanzo:

### Tahtmini ya hatari

Fomu ya tathmini ya hatari – CPJ: https://cpj.org/wp-content/uploads/2020/08/CPJ-Emergencies_Risk-Assessment-Template-2.pdf

Dondoo muhimu za usalama kwa waandishi wa habari kutoka African Centre for Media Excellence: https://acme-ug.org/wp-content/uploads/Essential-safety-tips-for-journalists-2.pdf

Miongozo ya usalama wa kidijitali – shirika la Reporters without border (RSF): https://resources.rsf.org/external-resources/

Eset (URL) Link Checker: https://www.eset.com/uk/home/link-checker/?srsltid=AfmBOo-q1GEKlvvr9V2uG-F4HjoULxxEytn3IGxqveoQLb11WWurGlpSh

Google URL checker: transparencyreport.google.com/safe-browsing/search

**Ushauri wa kisheria**

Vyanzo vya ushauri wa kisheria: https://resources.rsf.org/external-resources/

MiSA Tanzania: https://tanzania.misa.org/

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu Tanzania (Legal and Human Rights Centre Tanzania): https://humanrights.or.tz/en

Ulinzi wa Vyombo vya Habari (Media Defence): https://www.mediadefence.org/

Mtandao wa Sheria kwa Waandishi waliopo katika mazingira Hatarishi (Legal Network for Journalists at Risk): https://www.medialegalhelp.org/

**Sheria**

Elewa sheria za vyanzo vya taarifa kwa waandishi wa habari Tanzania - TRF and iWatch Africa: https://www.trust.org/wp-content/uploads/2025/07/KYRG-Tanzania-SOU-MAY-2025-V5-1.pdf

Sheria za Vyombo vya Habari Tanzania – Baraza la Habari Tanzania (Media Council of Tanzania): https://new.mct.or.tz/zlsc-constitution/

Miongozo ya Maadili – Baraza la Habari Tanzania (Media Council of Tanzania): https://new.mct.or.tz/zlscconstitutions/

## Majibu ya Zoezi 4.7

**Swali 1**. B ni sahihi. Ungependa kuongea na mhariri wako na kutathmini hatari na kuona kama ni mtu sahihi kwenda eneo hilo – inawezekana, kwa mfano, kuna mtu aliyepo karibu zaidi na eneo hilo.

**Swali 2**. Mapendekezo yote yanapaswa kuzingatiwa katika kutathmini hatari.

**Swali 3**. Hizi ni taarifa mpya muhimu sana kwa habari yako. Ni jambo gani la kwanza utafanya? Jibu sahihi ni A. Habari mpya inaleta hatari mpya ambazo unapaswa kuzitathmini. Unaweza kujiingiza hatarini kama utakwenda tu kwenye tukio peke yako bila kumwambia mtu au kujua nani utakwenda kuongea naye. Pia huna uthibitisho kuwa taka sumu zipo kwenye mfumo wa usambazaji maji safi ya eneo hilo – unatakiwa kupata sampuli kwa ajili ya kupima. Mara nyingi taarifa hubadilika katika mazingira husika, hasa pale hali ya hewa mbaya inapojitokeza hivyo hupaswi kupuuzia.

**Swali 4**. B na C ni majibu sahihi. Kama kuna uwezekano wowote wa kwamba mfumo wa usambazaji maji wa eneo hilo umechafuliwa na sumu, unapaswa kuhakikisha kuwa haunywi maji hayo kwani unaweza kuugua. Mara zote tembea na maji yako ya chupa wakati wa kuandika habari na unapaswa kuingiza hilo katika tathmini yako ya hatari unazoweza kukabiliana nazo. Nguo zako zinaweza kuchafuliwa na sumu hivyo mara zote beba nguo za kubadilisha na viatu na hakikisha nguo zilizochafuliwa na sumu zinafungwa kwenye mfuko wa plastiki.

**Swali 5**. B, C, D na E ni majibu sahihi. Usitegemee uzoefu wako pekee, usiamini kuwa mambo yataenda vizuri tu. Huduma za dharula zinaweza kutoa mwongozo wa jumla; wakati mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) yanaweza kuchukua hatua za haraka ili kukabiliana na majanga na yanaweza kuwa chanzo cha mawasiliano muhimu.

**Kiambatanisho cha 1**

## Wasikilizaji/watazamaji wangu ni nani? Maswali ya Utafiti

| Swali | Jibu |
|---|---|
| Je umri wa wasikilizaji/watazamaji wangu ni upi kati ya huu? | Chini ya miaka 18<br>18-25<br>26-35<br>36-50<br>51-64<br>Zaidi ya miaka 65 |
| Je wasikilizaji/watazamaji wako ni wa Jinsia ipi? | Me<br>Ke<br>Wote Me na Ke |
| Je wasikilizaji/watazamaji wako ni wa vijijini au Mjini? | Vijijini tu<br>Mijini tu<br>Kote |
| Je hali yao ya ajira ikoje? | Ameajiliwa kwa mkataba wa kudumu au amejiajili<br>Kwa sasa hajaajiliwa<br>Mwanafunzi<br>Anajishughulisha na kazi za nyumbani<br>Amestaafu |
| Kiwango chake cha elimu ni kipi? | Mpaka miaka 11<br>Mpaka miaka 16<br>Mpaka miaka 18<br>Ana elimu ya Shahada ya Kwanza na kuendelea |
| Hali ya familia ikoje | Mzazi ana Watoto ambao bado wako shule za awali<br>Mzazi ana Watoto wanaokwenda shule<br>Mzazi ana Watoto ambao ni watu wazima<br>Bibi na Babu wanawatunza watoto<br>Bibi na Babu hawawatunzi watoto<br>Ni mtu ambae hana mtoto |
| Je hali yao ya mahusiano ikoje? | Yupo mwenyewe<br>Ameoa/Ameolewa<br>Yupo kwenye mahusiano<br>Mjane/Mgani |

**Kiambatanisho cha 2**

## Fomu ya Tathmini ya Hatari

**Hatari** – andika hatari ya mtu mmoja mmoja ambayo unaweza kukabiliana nayo wakati wa kuandaa habari
**Uwezekano wa kutokea** – katika kila hatari andika uwezekano wa kutokea kwake. Inaweza kuwa hakuna uwezekano, kuna uwezekano, kuna uwezekano mkubwa
**Athari** – andika athari inayoweza kukupata, timu yako au vyanzo vyako vya taarifa kama hatari ikitokea katika uhalisia
**Mpango wa utekelezaji** – andika nini utafanya kama ukikabiliwa na hatari hii

| Hatari | Uwezekano | Athari | Mpango wa utekelezaji |
|---|---|---|---|
| ***Mfano:*** *Kukwama katika maji ya mafuriko na kushindwa kufika unakoenda* | *Kuna uwezekano* | *Kubwa* | *Kuchukua ushauri wa kupita kwenye njia salama zaidi. Kuhakikisha gari linafaa kutembea barabarani na lina bima kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza. Beba chakula cha akiba, maji na nguo za kujikikinga na mvua. Andaa simu za ufuatiliaji kwa mhariri wako.* |
| ***Mfano:*** *Polisi inaingilia kati mambo yako kwa kufanya ufuatiliaji (surveillance)* | *Hakuna uwezekano* | *Mbaya* | *Mwambie mhariri mara tu unapokuwa mbali na hatari hiyo. Ondoka katika eneo mara moja.* |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**Kiambatanisho cha 3**

## NYARAKA ZA KISHERIA ZILIZOREJELEWA

1. **Muundo wa Kikatiba**
   - Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ( Kama ilivyo fanyiwa marekebisho)
2. **Muundo wa Udhibiti wa Vyombo vya Habari**
   - Sheria ya Huduma za Habari
   - Kanuni za Huduma za Habari ( kama zilivyofanyiwa Marekebisho)
3. **Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Mamlaka ya Ukamataji**
   - Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai
   - Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi
4. **Udhibiti wa Mtandao na Kidijitali**
   - Sheria ya Makosa ya Mtandao
   - Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta
5. **Sheria Ya Usalama wa Taifa na Utulivu wa Umma**
   - Sheria ya Usalama wa Taifa
   - Sheria ya Utulivu wa Umma
6. **Upatikanaji wa Taarifa**
   - Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa
7. **Ushahidi na Usiri**
   - Sheria ya Ushahidi
8. **Ulinzi wa Mtoto na Faragha**
   - Sheria ya Mtoto
   - Kanuni ya Adhabu
9. **Viwango vya kimataifa vya nyongeza (supplementary international standards) ni viwango vya kisheria vinavyotolewa na mashirika ya kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa (UN), Shirika la Biashara Duniani (WTO), au Shirika la Kazi Duniani (ILO). Hata hivyo, viwango hivi havina nguvu ya moja kwa moja ya kisheria katika nchi wanachama**
   - Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu
   - Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa